ORODHA YA WAJUMBE WA BARAZA LA WAWAKILISHI
ZANZIBAR

MHE. PANDU AMEIR KIFICHO - SPIKA

1.Mhe. Balozi Seif Ali Iddi	MBM/Makamo wa Pili wa Rais/Kuteuliwa na Rais
2.Mhe. Dr. Mwinyihaji Makame Mwadini	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi/Jimbo la Dimani.
3.Mhe. Omar Yussuf Mzee	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais, Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo/ Kuteuliwa na Rais
4.Mhe. Haji Omar Kheri	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais, Utumishi wa Umma na Utawala Bora/Jimbo la Tumbatu
5.Mhe. Fatma Abdulhabib Fereji	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais/Kuteuliwa na Rais
6.Mhe. Mohammed Aboud Mohammed	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Makamo wa Pili wa Rais/Kuteuliwa na Rais
7.Mhe. Abubakar Khamis Bakary	MBM/Waziri wa Katiba na Sheria/Jimbo la Mgogoni.
8.Mhe. Rashid Seif Suleiman	MBM/Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano/Jimbo la Ziwani.
9.Mhe. Ali Juma Shamuhuna	MBM/Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Jimbo la Donge
10.Mhe. Juma Duni Haji	MBM/Waziri wa Afya/Kuteuliwa na Rais
11.Mhe. Zainab Omar Mohammed	MBM/Waziri wa Ustawi wa Jamii na Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto/Kuteuliwa na Rais
12.Mhe. Said Ali Mbarouk	MBM/Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo/Jimbo la Gando
13.Mhe. Ramadhan Abdalla Shaaban	MBM/Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati/Kuteuliwa na Rais
14.Mhe. Suleiman Othman Nyanga	MBM/Waziri wa Kilimo na Maliasili/Jimbo la Jang'ombe
15.Mhe. Nassor Ahmed Mazrui	MBM/Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko/Jimbo la Mtoni
16.Mhe. Abdillah Jihad Hassan	MBM/Waziri wa Mifugo na Uvuvi/Jimbo la Magogoni
17.Mhe. Haroun Ali Suleiman	MBM/Waziri wa Kazi, Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika/Jimbo la Makunduchi
18.Mhe. Mansoor Yussuf Himid	MBM/Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Kiembesamaki
19. Mhe. Haji Faki Shaali	MBM/ Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Mkanyageni
20.Mhe. Machano Othman Said	MBM/Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Chumbuni.
21.Mhe. Othman Masoud Othman	Mwanasheria Mkuu
22.Mhe. Issa Haji Ussi	Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano/Jimbo la Chwaka

23.Mhe. Zahra Ali Hamad	Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Nafasi za Wanawake
24.Mhe. Dr. Sira Ubwa Mamboya	Naibu Waziri wa Afya/Kuteuliwa na Rais
25.Mhe. Bihindi Hamad Khamis	Naibu Waziri wa Habari,Utamaduni,Utalii na Michezo/ Nafasi za Wanawake
26.Mhe. Haji Mwadini Makame	Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati/Jimbo la Nungwi
27.Mhe. Thuwaybah Edington Kissasi	Naibu Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko/Jimbo la Fuoni
28.Mhe. Abdalla Juma Abdalla	Jimbo la Chonga
29.Mhe. Abdalla Moh'd Ali	Jimbo la Mkoani
30.Mhe. Abdi Mosi Kombo	Jimbo la Matemwe
31.Mhe. Ali Abdalla Ali	Jimbo la Mfenesini
32. Mhe. Ali Mzee Ali	Kuteuliwa na Rais
33. Mhe. Ali Salum Haji	Jimbo la Kwahani
34.Mhe. Amina Iddi Mabrouk	Nafasi za Wanawake
35. Mhe. Asaa Othman Hamad	Jimbo la Wete
36.Mhe. Asha Abdu Haji	Nafasi za Wanawake
37.Mhe. Asha Bakari Makame	Nafasi za Wanawake
38.Mhe. Ashura Sharif Ali	Nafasi za Wanawake
39.Mhe. Bikame Yussuf Hamad	Nafasi za Wanawake
40.Mhe. Farida Amour Mohammed	Nafasi za Wanawake
41.Mhe. Fatma Mbarouk Said	Jimbo la Amani
42.Mhe. Hamad Masoud Hamad	Jimbo la Ole
43.Mhe. Hamza Hassan Juma	Jimbo la Kwamtipura
44.Mhe. Hassan Hamad Omar	Jimbo la Kojani
45.Mhe. Hija Hassan Hija	Jimbo la Kiwani
46. Mhe. Hussein Ibrahim Makungu	Jimbo la Bububu
47.Mhe. Ismail Jussa Ladhu	Jimbo la Mji Mkongwe
48.Mhe. Jaku Hashim Ayoub	Jimbo la Muyuni
49.Mhe. Kazija Khamis Kona	Nafasi za Wanawake

50.Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa Jimbo la Kikwajuni

51.Mhe. Makame Mshimba Mbarouk Jimbo la Kitope

52.Mhe. Marina Joel Thomas Kateuliwa na Rais

53.Mhe. Mbarouk Wadi Mussa Jimbo la Mkwajuni

54.Mhe. Mgeni Hassan Juma Nafasi za Wanawake

55.Mhe. Mlinde Mbarouk Juma Jimbo la Bumbwini

56.Mhe. Mohammed Haji Khalid Jimbo la Mtambile

57.Mhe. Mohammed Mbwana Hamad Jimbo la Chambani

58.Mhe. Mohammed Said Mohammed Jimbo la Mpendae

59.Mhe. Mtumwa Kheir Mbarak Nafasi za Wanawake

60.Mhe. Mussa Ali Hassan Jimbo la Koani

61. Mhe. Mohamedraza Hassanali Mohamedali Jimbo la Uzini

62.Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa Nafasi za Wanawake

63.Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi Nafasi za Wanawake

64.Mhe. Nassor Salim Ali Jimbo la Rahaleo

65.Mhe. Omar Ali Shehe Jimbo la Chake-Chake

66.Mhe. Panya Ali Abdalla Nafasi za Wanawake

67.Mhe. Raya Suleiman Hamad Nafasi za Wanawake

68.Mhe. Rufai Said Rufai Jimbo la Tumbe

69.Mhe. Saleh Nassor Juma Jimbo la Wawi

70.Mhe. Salim Abdalla Hamad Jimbo la Mtambwe

71.Mhe. Salma Mohammed Ali Nafasi za Wanawake

72.Mhe. Salma Mussa Bilali Nafasi za Wanawake

73.Mhe. Salmin Awadh Salmin Jimbo la Magomeni

74.Mhe. Shadya Mohamed Suleiman Nafasi za Wanawake

75.Mhe. Shamsi Vuai Nahodha Jimbo la Mwanakwerekwe

76.Mhe. Shawana Bukheti Hassan Jimbo la Dole

77.Mhe. Subeit Khamis Faki Jimbo la Micheweni

78.Mhe. Suleiman Hemed Khamis	Jimbo la Konde
79.Mhe. Ussi Jecha Simai	Jimbo la Chaani
80.Mhe. Viwe Khamis Abdalla	Nafasi za Wanawake
81.Mhe. Wanu Hafidh Ameir	Nafasi za Wanawake
Ndugu Yahya Khamis Hamad	**Katibu wa Baraza la Wawakilishi**

Kikao cha Sita – Tarehe 17 Oktoba, 2012

(Kikao kilianza saa 3:00 asubuhi)

DUA

Mhe. Spika (Pandu Ameir Kificho) alisoma dua

MASWALI NA MAJIBU

Nam. 47

Upungufu wa Vituo vya Huduma ya Uzazi

Mhe. Jaku Hashim Ayoub – Aliuliza:-

Kadri ya idadi ya watu inavyoongezeka kila mwaka, ndivyo watoto wengi huzaliwa kila siku katika hospitali zetu.

(a) Je, hatuoni kwamba vituo vya akinamama vya kujifungua kwa sasa havitoshi.

(b) Serikali ina mpango gani wa kuongeza vituo hivyo katika maeneo mbali mbali ya nchi yetu.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya – Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 47 lenye vifungu a na b kwa pamoja kama hivi ifuatavyo:-

a) Mhe. Spika, baada ya jitahada kubwa ya watendaji wa afya kupitia kitengo shirikishi cha Mama na Mtoto kuwafahamisha wajawazito umuhimu wa kuhudhuria kliniki na kuzalia hospitali, na pia kutolewa agizo la Rais kuwa huduma za uzazi ni bure, inaonekana kina mama wamehamasika kuzalia hospitali na kufanya mahospitali na vituo kuzidiwa.

b) Kwa kuliona hilo wizara imeamua kwa makusudi kuhakikisha kuzisogeza huduma hizo karibú na wananchi. Wizara imeanza mchakato wa kuangalia na kupanga utaratibu wa kuviwezesha vituo mbali mbali kuzalisha huku tukiangalia ufikwaji kwa urahisi kwa waja wazito unapofika muda wao wa kujifungua. Lengo kuu la wizara linalotaka kufikia ni kuona kila panapo kituo cha afya basi huduma ya kuzalisha inakuwepo

Mhe. Spika, ili lengo hili lifikiwe kuna mambo mengi yanahitaji kuwekwa sawa ili mafanikio yapatikane yakiwemo:

1. Kuongeza nguvu kazi kwa kuchukua idadi kubwa ya wanafunzi wauguzi wakunga ili hatimae kufanya kila kituo kiwe na mfanyakazi anayeweza kuzalisha.

2. Kuengeza idadi ya vituo vinavyotoa huduma ya kuzalisha kwa awamu mpaka mpango mzima kukamilika kwa kila kituo kuzalisha.

3. Kuhamasisha kujenga nyumba za wafanyakazi kila panapo kituo cha afya ili muuguzi mkunga aweze kuishi karibú na kituo na apatikane saa anapohitajika.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri yaliyokidhi swali la msingi naomba nimuulize maswali ya ziada. Hivi karibuni kumetokea tatizo kubwa linalohusu sehemu ya upasuaji katika Kisiwa cha Pemba katika Hospitali ya Chake Chake na kusababisha mama mjamzito huyo kupoteza mtoto tokea kufika hospitali muda wa saa tatu mpaka saa sita na nusu hajapokelewa hospitali hapo. Na yeye mwenyewe ni

shahidi alikwenda kwa kutumwa na waziri kuona tukio hilo. Je, haoni umefika wakati wa kuweka daktari bingwa masaa 24 katika hospitali hiyo pamoja na hospitali za *cottages*, ili kufanikisha kilio cha wanyonge wa nchi hii ambacho Mhe. Rais alikipokea na kuamuru au kutoa fursa kwa wajawazito wote kujifungua bure.

Pili, kwa kuwa Hospitali ya Chake Chake ina umuhimu mkubwa katika vitongoji, sababu gani zilizopelekea hata ikafikia kuwa taa za upasuaji zikaungua zote na hivi sasa hali hiyo inaikabili pia Hospitali ya Mnazi Mmoja kutokana na ukosefu wa *Operating Theater Lamp*. Je, wizara yake imejifunza nini.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya: Mhe. Spika, kuhusu huyo mzazi anayemzungumza Mhe. Jaku Hashim ni mwanamama wa miaka 35 anayekaa Vitongoji ambaye alikuwa mja mzito mimba ya tano na alikuwa anakwenda kliniki na wakakuta kwamba mtoto hakulala vizuri, alishauriwa aende Hospitali ya Chake Chake kwenda kuzalia. Mwanamama huyo alipopata uchungu kwa siku mbili hakwenda katika kituo cha afya hata kilichokaribu naye hapo Vitongoji pia hakwenda, amekaa mpaka mkono umetoka nje ndipo walipomchukua wakampeleka Vitongoji Hospitali tena kinachoshangaza ni mke wa Diwani.

Mimi nilitegemea kwamba Diwani atafanya kila liwezekanalo kwa sababu ni muelewa na ni kiongozi kuhakikisha kwamba mkewe anakwenda hospitali, lakini hakwenda. Alipofika hospitali Vitongoji wamefika saa tisa mchana, Vitongoji wakawasiliana na Hospitali ya Chake Chake wakawakuta siku hiyo kulikuwa kuna kambi na kunafanyika operesheni, walichowaambia watu wa Chake Chake fanyeni matayarisho yote mumlete mgonjwa tutakapokuwa kambi imemalizika saa 12 tuhakikishe kwamba mgonjwa amefika hospitali.

Kwa hivyo, kunako saa kumi wakaanza kumhudumia yule mgonjwa kuchukua vipimo vya damu na kila kitu, kufika saa 12 wakamchukua wakampeleka Hospitali ya Chake Chake na walipofika watu wametoka kwenye kambi na wamekwenda kula chakula baada ya kufanya kazi kwa masaa 12 siku ile. Walipotoka kula chakula wakaja pale wakahakikisha na walifika pale saa tatu kutoka Vitongoji na saa tano juu ya alama mgonjwa yule amefanyiwa operesheni mtoto akatolewa na alipotolewa mtoto alikwishakufa na ametolewa tayari mtoto ameshaanza kunyambukanyambuka. Kwa sababu sio jambo la siku moja, baada ya hapo mgonjwa akahudumiwa akapelekwa wodini, mgonjwa mzima.

Siku ya Pili Diwani mwenyewe na baba yake mgonjwa wakenda Hospitali ya Chake Chake wakasema wanataka mgonjwa wao arudishwe Vitongoji, wakaambiwa haitowezekana kwa sababu Vitongoji hakuna daktari wa kwenda kumhudumia tunataka mgonjwa huyu abaki hapa mpaka atakapopona.

Mimi nimekwenda Pemba nimekutana na huyo mama akaeleza kadhia hizo kama ilivyokuwa, nikamuuliza ulipofika hapa Chake Chake hukupokelewa? Akanambia nimepokelewa. Huduma uliyoipata akanambia nimefanyiwa operesheni na ninashukuru *Alhamdulillah* sijambo, nikamuuliza ulidhalilishwa hapa ulipofika hukushughulikiwa? Akanambia kila kitu nimefanyiwa isipokuwa nakuomba jambo moja tu, wafanyakazi hapa mama hawatoshi wasaidie, nikamwambia hilo nalijua na tutalifanyia kazi. Kwa hivyo, mgonjwa hakudharauliwa wala hatukuuwa mtoto, mtoto alikufa tangu kwao.

Swali la pili analolizungumzia ni suala la *theater* kuwa hakuna taa. Juzi nilisema Mhe. Spika, kwamba taa zimeshakuweko na zimeshatiwa na taa za *theater* sio moja, kwenye mzunguuko kuna taa nane taa moja ikiharibika na nyengine hazihimili kwa hivyo, itaungua moja baada ya nyengine na huwezi ukabadilisha taa moja na Pemba taa hazipatikani sio kama *bulb* za nyumbani. Kwa hivyo, ina maana mpaka ziagiziwe, zimeagiziwa zimeletwa mzunguko mzima ambao una taa nane na umeshabadilishwa. Kwa hivyo, hivyo vitu vinatokea kwani jamani vitu vya *electronic* haviharibiki? Kwa nini ikiwa vinaharibika Wizara ya Afya tu ndio inakuwa *issue*, majumbani taa haziungui?

UTARATIBU

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Spika, mimi ushahidi wa hilo na yeye alipopigiwa simu niko kwenye kamati ya Ustawi wa Jamii, Wanawake na Watoto, Mhe. Waziri akampigia simu akaambiwa alifuatilie hilo suala. Mimi kuanzia saa tatu nilipokea simu kutoka Pemba mgonjwa kafika saa tatu mpaka sita na nusu hajapokelewa hapana daktari dhamana pakawa pana upungufu wa mafuta na mimi nikawaambia kama hapana mafuta naomba nikopeshwe mpaka siku ya pili asubuhi nitazileta pesa hizo, akachukuliwe Mkoroshoni daktari kuja kumshughulikia. Swali langu mimi kutoka saa tatu mpaka sita na nusu hakuna daktari dhamana? Hakupata huduma hiyo na ikasababisha mtoto

kupoteza maisha, hata mwenyewe angepoteza maisha kwa hivyo bado hatujawa *serious* na hilo, Mhe. Naibu Waziri naomba alikubali hilo.

Mhe. Spika: Kwa hivyo, suala ni daktari dhamana kutokuwepo.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Swali ni kuwa kutoka saa tatu mpaka sita na nusu hawajampokea hapana daktari dhamana mpaka nikampigia Afisa Mdhamini Pemba anaitwa Ukasha yuko chuoni akamtafuta daktari anaitwa Yussuf kama sikosei ndio baadae akahudumiwa, kama hatukuingia kati sisi ingekuwa hatari kubwa Mhe. Spika Mwenyezi Mungu atunusuru.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya: Mhe. Spika, kama nilivyosema tunajua kwamba Pemba wafanyakazi ni wachache Daktari dhamana na madaktari wengine wote walikuwa kwenye kambi, kambi hiyo ilikuwa ni ya upasuaji hivyo huwa inajumuisha wafanyakazi wote wa afya walioko pale ni mmoja mmoja tu anayekuweko wodini, lakini mawasiliano baina ya Vitongoji yamefanyika mgonjwa kahudumiwa. Na yeye kwanza anasema uongo, kwa sababu hili jambo lilizungumzwa alipokuwa kwenye Kamati Tendaji walipokuwa Wizara ya Afya na Waziri wa Afya akapiga simu na alipopiga simu mimi nilikuwa Pemba. Waziri wa Afya akanambia kwamba Kamati Tendaji imekwenda Pemba nikasema Kamati Tendaji Pemba haikwenda kwa sababu Kamati Tendaji itakwenda Pemba mwezi wa 12, umesema uongo. *(Makofi)*

(Hapa Mhe. Jaku Hashim alisimama na kutaka kuanza kusema)

Mhe. Spika: Mhe. Jaku Hashim hujapewa nafasi ya kusema utaendelea kusema vipi bwana. Tunakwenda kwa utaratibu, inawezekana Mhe. Waziri amekuwa mkali sana kusema kwamba umesema uongo. Hiyo inawezekana na basi niombe radhi kuhusiana na hilo. Lakini kimsingi majibu ameshatoa kwamba kilichotendeka ni kuwa madaktari wote walikuwa kwenye kambi ndio tatizo lililofanya ikabidi masuala yote yamechelewa na kambi hiyo nayo ilikuwa ina maana maalum kwa ajili ya kulinda afya za wananchi. Nadhani suala hili limemalizika.

Mhe. Nassor Ali Salim: Ahsante sana Mhe. Spika, kwa kunipa nafasi hii ya kuuliza swali moja la nyongeza. Kwanza nichukue fursa hii kumpongeza Mhe. Naibu Waziri kwa majibu yake mazuri ya kiutaalamu yenye kueleweka. Mhe. Spika, katika hospitali ambazo husaidia sana kupunguza matatizo ya kinamama na watoto ni Hospitali ya Mwembeladu ambayo iko katika jimbo la Rahaleo. Mhe. Spika, hospitali ile husaidia majukumu mengi pia mengine huyabeba Hospitali ya Mnazi Mmoja. Je, wizara ina mpango gani wa kuboresha huduma za kinamama na mtoto katika kusaidia tatizo hili.

Pili, Hospitali ya Mwembeladu ina madaktari bingwa wangapi na kama haina wizara ina mpango gani kuweka daktari bingwa katika hospitali ile.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya: Mhe. Spika, kama anavyosema kuwa Hospitali ya Mwembeladu iko kweli katika Jimbo lake na inahudumia wazazi tu, haihudumii wagonjwa wengine. Na Hospitali ya Mnazi Mmoja ndio hospitali nyengine ambapo inahudumia wazazi. Katika mipango ambayo tunaipanga kwa hivi sasa ni kuhakikisha kwamba tunakamilisha Hospitali ya Kwamtipura ili kliniki zote zilizoko pale chini katika Hospitali ya Mwembweladu zihamie Kwamtipura na Hospitali ya Mwembeladu yote nzima iwe ni hospitali ya kuzalisha ili uzazi wa kawaida wowote ule utakaokuja ufikie Mwembeladu na Mnazi Mmoja waende wale tu watakaohitaji huduma ambazo ni zaidi ya kuzaa kwa lazima.

Lakini Hospitali ya Mwembeladu hivi sasa ina daktari bingwa mmoja ambaye ametoka China na daktari mwengine ambaye ni daktari bingwa pia lakini ni daktari wa uzazi wa mpango katika kitengo anasaidiana na daktari huyo kufanya kazi katika hospitali ile.

Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi: Ahsante sana Mhe. Spika, naomba kwanza Mhe. Naibu Waziri anijibu vizuri na nifahamu vizuri. Kwa kuwa Mkoa wa Kusini Pemba katika kituo cha Kangani kituo kile ni kidogo na kwa kuwa eneo lile ni kubwa wanaishi wananchi wasiopungua 2,000 na kwa kuwa wananchi wale wana matatizo ya kujifungua katika kituo kile. Je, Mhe. Naibu Waziri kuna mpango gani wa kwenda kukiona kwanza kile kituo na ikiwezekana ikaongezwa nafasi ili wananchi wajifungulie pale badala ya kwenda kujifungulia katika hospitali kuu ya Mkoani.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya: Mhe. Spika, wakati nilipokuwa Pemba wiki tatu zilizopita tulikuwa tunafanya *mathing* ya kuona jinsi gani na vituo vipi ambavyo tutavipa kipaumbele ili viweze kuzalisha Mwanza. Tumeangalia kwa kutizama uwezo wa kuweza kufika kwenye kile kituo na umbali wa kituo chengine na tukatambua baadhi ya vituo. Kama kituo cha Kangani kwa karibu hapana kituo ambacho kinazalisha hivyo vituo vyote vitapandishwa daraja, vitajengwa upya, lakini tatizo letu litabaki kama hakuna nyumba pale sisi pesa za kujengea nyumba hatuna na ili kituo kiweze kuzalisha saa 24 ina maana pale pawe na mkunga karibu.

Sasa Wawakilishi nakuombeni jitahidini basi mpate hizo nyumba na sisi tutimize wajibu wetu. Lakini nitaliangalia zaidi kukuhakikishia kwamba kituo cha Kangani kama kimo nitakwambia na kama hakipo nitakwambia ni kituo gani ambacho wananchi wa Kangani wataweza kufika. Kwa sababu hatufanyi kwanza moja kwa moja kila kituo isipokuwa tunaangalia jografia ya sehemu ile kuhakikisha wananchi wengi wanafika katika eneo husika kuweza kujifungua.

Baada ya hapo mpango wa Pili tutamaliza vituo vyote ambavyo vipo vya *second line* ambavyo vinatakiwa kuzalisha. Mpango wa tatu tutahakikisha kwamba vituo vyote vya Unguja na Pemba huduma ya kuzalisha inapatikana. Kwa hivyo, kama hawamo katika mpango wa kwanza watakuwa katika mpango wa pili, kama hawamo katika mpango wa pili watakuwa kwenye mpango wa tatu.

Nam. 61

Vituo vya Daladala

Mhe. Jaku Hashim Ayoub – Aliuliza:-

Ahsante sana Mhe. Spika, kabla ya kujibiwa swali langu naomba uniruhusu niseme machache. Kwa kweli mimi nimedhalilishwa na Naibu Waziri wa Afya, mimi nimechaguliwa na wananchi wa Jimbo la Muyuni wakisikia kuwa nasema uongo Barazani itakuwa imenivunjia heshima sana Mhe. Spika kwa unyonge wa hali ya juu. Sisi tumekula kiapo kuwatumikia wananchi na kusema uongo Wajumbe wako ni mwiko humu ndani, niliyozungumza yote nilikuwa na uhakika nayo.

Baada ya hapo Mhe. Spika, naomba nijibiwe swali langu nambari 61.
Mji wa Zanzibar kwa muda mrefu hakuna vituo maalum vya daladala na kusababisha gari kusimama ovyo hasa katika njia ya Uwanja wa Ndege, Kiembesamaki, Chukwani, Bububu na maeneo mengine ya Manispaa.

(a) Je, Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano ina mpango gani wa kuweka vituo maalum na viwango vya nauli kulingana na umbali wa safari ya abiria.

(b) Kwa nini abiria wanaoanza safari katikati wamekuwa wakitozwa nauli sawa na abiria aliyepanda gari mwanzo wa safari.

Mhe. Spika: Kabla sijamuomba Mhe. Naibu Waziri kujibu mimi nililiona mapema nikasema kwamba Mhe. Naibu Waziri amekuwa mkali kidogo na ameteleza kusema kwamba unasema uongo, ni udhaifu wa kibinadamu na basi nichukue nafasi hii kwamba hilo liwe limekwisha tusogee mbele tufanye mengine, lakini ni udhaifu wa kibinadamu. Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano njoo ujibu swali.

Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano – Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa rukhsa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake nambari 61 lenye vifungu (a) na (b) kama hivi ifuatavyo:-

Mhe. Spika, ni kweli kwamba kwa muda mrefu katika mji wa Zanzíbar yapo baadhi ya maeneo hakuna vituo maalum vya daladala na hivyo husababisha magari kusimama ovyo katika maeneo ya barabara, lakini pia yapo baadhi ya maeneo hasa katika njia ya bububu bado huduma za vituo hivyo zipo. Baada ya maelezo hayo mafupi Mhe. Spika, sasa naomba kumjibu Mhe. Mjumbe kama ifuatavyo:-

(a) Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano katika kipindi cha miaka miwili sasa hivi imo katika maandalizi ya mradi mkubwa wa upanuzi wa barabara za mjini ili kuweka sehemu maalum kwa ajili ya vatu wanaopanda na kushuka katika huduma ya usafiri barabarani, lakini pia kutanua barabara hizo pamoja na kuzingatia maeneo maalum ya matumizi zikiwa pamoja na zile *pavement* na maeneo ya kupita kwa vatu wenye ulemavu.

(b) Mhe. Spika, kama nilivyojibu katika suala la (a) abiria wanaosafiri katika masafa yasiozidi maili sita wanatozwa nauli sawa hata kama ameianza safari hiyo katikati ya safari. Sababu ya kufanya hivyo ni kuwa maudhui makubwa ya safari za daladala ni kwa ajili ya masafa mafupi katika maeneo ya miji. Kwa hivyo, kama maeneo yale yako katika maili sita atakae panda daladala katika eneo la maili tatu atapaswa kutozwa nauli sawa na yule ambaye amepanda kwa eneo lote la maili sita.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri pamoja na serikali kuwa na mpango wa kutanua barabara ningemuomba Mhe. Naibu Waziri angalau wakaweka japo vibao baadhi ya sehemu kutokana na daladala kusimama ovyo, angalau vibao tu ambavyo havina gharama kubwa. Kwa ushahidi huo ninaosema hivi sasa njia ya kwendea Uwanja wa Ndege nyumbani pa Mhe. Dr. Salmin Amour pamewekwa kituo cha daladala buba pale mlangoni pa Mheshimiwa.

Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Spika, katika baadhi ya maeneo wazo hilo la Mhe. Mwakilishi nalipokea na tunacho waomba wananchi kwamba vile vibao au alama zilizowekwa basi nao washirikiane nasi katika kuvitunza na tunaamini kwa ushirikiano wetu sisi, Manispaa na Halmashauri tutaweza kulichukua wazo hilo na kulifanyia kazi haraka iwezekenavyo ili kunusuru usumbufu wanaoupata wananchi wetu.

Mhe. Ali Salum Hají: Ahsante Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri kwanza kabla sijauliza swali langu nimpongeze Mhe. Naibu Waziri kwa jitihada ambayo imeanza kuonekana katika Manispaa ya Zanzíbar zile kelele zetu zinaanza kufanyiwa kazi, maeneo ya wanaopita kwa miguu, maeneo ya *parking* na maeneo mbali mbali yameanza kufanyiwa marekebisho. Lakini naomba nimuulize swali langu dogo tu. Pamoja na maelezo yake kwamba wamo katika mradi wa kutaka kupanua barabara hizo na kujenga vituo vya ku-*park* gari kwa ajili ya upakizi wa abiria. Naomba anieleze Mhe. Naibu Waziri ana jitihada gani za dharura za kuweza kuondosha usumbufu wa kituo cha daladala cha Michenzani ambapo kipindi kikubwa kinapelekea magari kusimama barabarani na kutoa usumbufu kwa magari mengine kutoweza kupita katika eneo hilo.

Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Spika, ni kweli kwamba katika maeneo ya Michenzani kumekuwa na usumbufu mkubwa unaotokana na magari ku-*park* pasina utaratibu unaoeleweka, lakini sisi wizara yetu kwa kushirikiana na wenzetu wa Manispaa tumeweza kufanya jitihada za kushirikiana na wenzetu Jeshi la Polisi hasa Kitengo cha Usalama Barabarani, naamini Mhe. Mwakilishi akiwa mpelelezi kwa muda wote wa masaa 12 pengine mpaka saa mbili za usiku kuna askari wa usalama barabarani wanaokaa eneo lile ili kunusuru hali hiyo ya usumbufu wa kuweza njia ile kuzuilika kutotumika kama ilivyokusudiwa.

Kwa hivyo, ombi lake Mhe. Mwakilishi tumelipokea na sisi wajibu wetu ni kuwakumbusha wenzetu wa polisi watimize wajibu wao kama vile ambavyo tumezungumza tukawa tumeelewana hapo awali. Madhumuni ya kukaa kwao pale ni kuondoa ule usumbufu wanaoupata wananchi wa magari ku-*park* kinyume na utaratibu.

Nam. 6

Kukataliwa kwa Nguzo za Umeme

Mhe. Saleh Nassor Juma - Aliuliza:-

Kwa kuwa wananchi wengi walinunua nguzo za umeme kwa ajili ya kupeleka umeme katika maeneo mbali mbali yakiwemo maeneo ya maduka ya mbao za kawaida. Na kwa kuwa Shirika la Umeme limezikataa nguzo hizo na kuwalazimisha wananchi kununua nguzo kutoka kwenye Shirika lao, ambazo ni ghali mno.

Je, ni sababu gani zilizopelekea kukataliwa kwa nguzo hizo.

Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati - Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 6 kama hivi ifuatavyo:-

Mhe. Spika, shirika limezikataa nguzo hizo kwa sababu hazikua na ubora wa kupikika kwa dawa ya kuzuwia kuliwa na wadudu jambo ambalo husababisha kuoza kwa nguzo hizo na kuanguka na kuhatarisha maisha ya wananchi.

Mhe. Saleh Nassor Juma: Ahsante sana Mhe. Spika, pamoja na majibu mafupi sana yasioridhisha aliyonijibu Mhe. Naibu Waziri naomba kuuliza swali la nyongeza lenye kipengele a na b.

(a) Kwa kuwa Shirika la Umeme ni shirika linalomilikiwa na Serikali yetu ya Mapinduzi ya Zanzíbar, na kwa kuwa shirika hili linakwenda na kufanya shughuli zake kupitia kodi za wananchi, na kwa kuwa nguzo hizo nyingi zimetiwa dawa. Je, isingekuwa vyema shirika hilo likazikubali nguzo hizo au kupeleka nyengine kwa gharama zake wenyewe.

(b) Kuzikataa nguzo hizo na hatimaye wananchi kuendelea kukosa huduma ya umeme katika maeneo kadhaa likiwemo eneo la Vitongoji Umangani. Je, si kuwakosesha wananchi matunda ya Mapinduzi Matukufu ya mwaka 1964 yaliyoongozwa na Mheshimiwa Muasisi wa nchi hii Marehemu Abeid Amani Karume.

Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati: Mhe. Spika, lengo la Shirika la Umeme Zanzíbar ni kuhakikisha kuzibadilisha nguzo zote ambazo mbovu na zote ambazo hazina kiwango. Mhe. Spika, naomba nimfahamishe Mheshimiwa kwamba wananchi wengi wametumia nguzo ambazo hazina kiwango kwa kipindi kirefu jambo ambalo mimi mwenyewe katika ufuatiliaji wangu nimelishuhudia hilo, kuna baadhi ya maeneo zimewekwa nguzo mpaka za Mikeshia, za Mipera na Mivinje, jambo ambalo limeitia shirika hasara kubwa mno kwa sababu nguzo hizo hazina ustahamilivu baada ya kutumika kwa kipindi cha mwaka mmoja au nusu mwaka basi nguzo hizo zinaanguka na kusababisha hatari kubwa sana ya kushuka laini za umeme na kusababisha hatari kwa wananchi wanaoishi katika maeneo hayo.

Nimhakikishie Mhe. Mwakilishi kwamba maeneo yote ambayo yana nguzo kama hizo mbovu basi shirika langu zitalishughulikia na kuhakikisha kwamba tunaweka nguzo nyengine mpya.

Mhe. Saleh Nassor Juma: Bado swali la (b) hajalijibu.

Mhe. Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati: Mhe. Spika, kwanza nataka kumtanabahisha Mhe. Mwakilishi kwamba amesema jibu lilikuwa fupi. Mhe. Spika, swali lake lilistahili kupata jibu fupi kwa sababu liliuliza, ni sababu gani zilizopelekea kukataliwa kwa nguzo hizo? Kwa hivyo, sababu Mhe. Naibu Waziri aliitoa na hakuwa na haja tena ya kuendelea na mazungumzo mengine.

La pili hili suala la kusema kwamba haoni kwamba kufanya hivyo itakuwa wananchi wa Zanzibar wanakoseshwa matunda ya Mapinduzi ya mwaka 1964. Ninamjibu kwamba wananchi wa Zanzibar hawakoseshwi matunda ya Mapinduzi mwaka 1964, na aangalie mwaka 1964 umeme usambazaji wake ulikuwa umeishia wapi na hivi sasa usambazaji wa umeme umeishia wapi. Karibu mashamba yote hivi sasa yana umeme na watu wengi hivi sasa katika nyumba zao wana umeme na ninashukuru ni kwamba kwa sababu hili tunda ni zuri hata wananchi hivi sasa wanahamasika kutengeneza nyumba nzuri, kwa sababu ukitia katika nyumba mbovu unakuumbua, siku unapouwashwa mabui bui unayaona, kiambaza hakikupendezi. Kwa hivyo unatengeneza kiambaza chako vizuri kabisa. Hivyo hawakoseshwi, kwa hivyo jitihada hii bado ipo lakini ninasema ni vizuri tushirikiane na Waheshimiwa katika kurekebisha nguzo, wao wanatembea hawa wanaona nguzo zinazoporomoka poromoka humu njiani, ni nguzo ambazo zimekuwa *treatment* lakini dawa yenyewe sio kuliko inayoweza kuzifanya nguzo zile zidumu kwa muda mrefu.

Kwa hivyo shirika linapata hasara kama alivyosema Mhe. Naibu Waziri kwa sababu inabidi kila mara wafanye *repair* ya nguzo, na ndio maana wakaamua ni bora kula hasara ya mara moja tukaepuka ule usemi wa Kiswahili kwamba karamu ya mbahili huliwa mara mbili.

Kwa hivyo tule hasara mara moja lakini nguzo idumu miaka sita, kumi, kumi na tano bila ya kuharibika. Ahsante sana Mhe. Spika. (*Makofi*).

Nam. 46

Kumbukumbu za Picha za Wageni Mashuhuri

Mhe. Jaku Hashim Ayoub – Aliuliza**:-**

Mhe. Spika, kwa vile mara tu baada ya Mapinduzi viongozi mbali mbali wa dunia walio maarufu walitembelea nchi yetu. Na kwa kuwataja badhi ya viongozi hao ni pamoja na Fidel Castro wa Cuba, Ahmed Benbella wa Algeria, Nelson Mandela wa Afrika Kusini na wengi wengineo.

Je, Idara husika ya habari inayo "*record*" ya tarehe na hata picha za viongozi hao katika makumbusho yetu wakati wa ziara zao hapa Zanzibar.

Mhe. Naibu Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo – Alijibu**:-**

Mhe. Spika, kwa idhini yako na kwa niaba ya ya Mhe. Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake nambari 46 kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika**,** Wizara yangu kupitia Idara ya Habari maelezo inazo kumbukumbu ya tarehe na hata picha za viongozi hao akina Mhe. Castro, Ben Bella wa Algeria na Mandela wa Afrika Kusini na viongozi wengine.

Hivi karibuni Serikali ya Misri kupitia ubalozi wake mdogo wa Zanzibar ulimuomba Makamu wa Pili wa Rais, picha za ziara ya Rais Gamal Abdul Nassir alipotembelea Zanzibar, na tuliweza kuwapatia kumbumbu na picha hiyo na kutupongeza.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Ahsante sana Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri, kwa nini picha hizo hazitumiki kwenye magazeti ya serikali kama tulivyoona kwenye magazeti ya Daily News na Habari Leo ili kunufaisha vizazi vijavyo kuona wana harakati wa ukombozi wa Afrika.

Mhe. Naibu Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo: Ahsante sana Mhe. Spika, naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake kama ifuatavyo.

Mhe. Spika, nakubaliana na Mhe. Mwakilishi lakini tumejipanga kwa sababu tunajua kwamba wananchi wetu wengi hasa vizazi vyetu vya leo hawawajui viongozi waliopita, kwa kweli tumejipanga vizuri na tutatoa kwenye magazeti na vyombo vyetu vya televisheni.

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Spika, baada ya majibu ya Mhe. Naibu Waziri naomba anielimishe.

Nchi yetu imepata uhuru kupitia Mapinduzi matukufu mwaka 1964 na viongozi baada ya Mapinduzi na baada mbio za kutaka umoja wa Afrika ni karibu hivi sasa miaka 40. Hebu Mhe. Naibu Waziri atwambie tuwagaie muda gani ili wajipange ili mambo haya yatoke kwenye Idara ya Habari Maelezo kwa sababu kama wanajipanga hivi leo, pengine angetwambia ni miaka mingapi watakuwa wamejipanga ili Wazanzibari wafaidike na kumbukumbu hizo za viongozi mashuhuri wa Afrika.

Mhe. Naibu Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo: Mhe. Spika, naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake la nyongeza kama ifuatavyo.

Mhe. Spika, kwa kweli nimeeleza vizuri lakini pia kwa sababu hawa si viongozi wa Zanzíbar ni viongozi wa nje kama nilivyokwambia tunajipanga vizuri na tutaweza kutoa kwenye vyombo vyetu vya televisheni na magazeti.

Mhe. Mwakilishi kwa kweli naomba hilo ukubaliane na mimi na wizara yangu.

Mhe. Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo: Mhe. Spika, nakushukuru na nimpongeze Mhe. Naibu Waziri kwa ufafanuzi wake mzuri, ila naomba niongeze majibu kwamba Zanzíbar tulikuwa na gazeti moja la Serikali yaani Zanzíbar Leo.

Sasa gazeti lile limekuwa na mambo mengi ndani yake, mambo ya kiuchumi, kimichezo, kihistoria. Sasa kwa kuliona hilo na haja ambayo Waheshimiwa Wawakilishi wamezungumza, hivi karibuni tumezindua gazeti jengine ambalo litaweza kidogo kuleta unafaa wa kurasa katika gazeti hili ambalo limekuwa lipo.

Kwa hivyo baada ya kujipanga huko ambako Mhe. Naibu Waziri amekutaja, sasa gazeti letu la Zanzíbar Leo litakuwa na nafasi ya kutosha kuwa na nafasi ya kuchapisha baadhi ya haja ambazo Waheshimiwa Wawakilishi wamezitaja.

Kwa hivyo masuala ya michezo, burudani, historia na utalii litakuwa na gazeti ambalo litasaidia katika kufanya hivyo. Huko ndiko ambako tumekusudia kujipanga zaidi.

Nam. 52

Mafunzo juu ya Utunzaji wa Miche ya Mikarafuu

Mhe. Jaku Hashim Ayoub - Alijibu**:**

Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imeamua kuimarisha zao la karafuu ambapo katika msimu uliopita miche 500,000 ilikuwa itolewe kwa wakulima.

(a) Je, Serikali imefanikiwa kutoa miche mingapi kwa wakulima.

(b) Kwa kuwa wakulima wengi hawana taaluma ya utunzaji miche na kusababisha mingi kufa. Je, Serikali imetoa taaluma kwa wakulima wangapi ambao wamenufaika na miche hiyo.

(c) Kwa kuwa Serikali iliahidi kufanya sensa ya miti ya mikarafuu Unguja na Pemba kama kazi hiyo imefanyika matokeo yanasemaje juu ya mikarafuu Zanzibar.

Mhe. Naibu Waziri wa Kilimo na Maliasili - Alijibu**:**

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 52 kama ifuatavyo kwa pamoja.

Mhe. Spika, kabla ya kumjibu Mhe. Mwakilishi aliyeuliza swali lenye kipengele (a), (b), na (c) naomba kutoa maelezo kama ifuatavyo.

Wizara yangu imefanikiwa kuzalisha miche 500,000 ya mikarafuu, kati ya hiyo jumla ya miche 349,335 imetolewa kwa wakulima wa Unguja na Pemba katika msimu wa mvua za masika kwa 2012. Aidha, wakulima binafsi nao wamehamasishwa na hatimaye kuzalisha miche 68,210 kwa matumizi yao na ziada kuwauzia wakulima wengine.

Mhe. Spika, mikarafuu iliyozalishwa na Wizara ya Kilimo na Maliasili imegawiwa kwa wakulima kama ifuatavyo:-

- Wilaya ya Kaskazini A - 34,833
- Wilaya ya Kaskazini B - 25,281
- Wilaya ya Kati - 45,629
- Wilaya ya Magharibi - 39,307
- Wilaya ya Kusini - 2,950
- Wilaya ya Mkoani - 67,300
- Wilaya ya Wete - 29,365

- Wilaya ya Micheweni - 19,635
- Wilaya ya Chake Chake - 85,035

Mhe. Spika, Wizara ya Kilimo na Maliasili imechukua jitihada kubwa katika kuwapatia elimu wakulima wa zao la karafuu na mazao mengine ya viungo na Matunda, kwa upande wa zao la mikarafuu jumla ya wakulima 206 walipatiwa mafunzo ya kuendeleza zao hilo katika nyanja zifuatazo:-

- Utayarishaji miche kitaluni pamoja na uchimbaji mahiri wa mabotea;
- Utayarishaji wa mashamba kabla na baada ya kupanda mikarafuu;
- Upandaji wa mikarafuu na palizi;
- Uwekaji wa matandazo (Mulching), uchumaji, ukaushaji na utayarishaji wa karafuu kabla ya kupelekwa sokoni

Mhe. Spika, Wizara ya Kilimo na Maliasili iliweza kutayarisha kipindi cha mkulima wa karafuu kwa njia ya T.V ili kuhamasisha wananchi na wakulima, pia tuliandaa utaratibu wa upandaji miti kitaifa ili kuamsha ari kwa wananchi kwa kuipanda na kuitunza mikarafuu ipasavyo, mfano wa mashamba yaliopandwa kwa siku hiyo ni Kizimbani na Kinumoshi kwa Unguja na Tungamaa na Mkanyageni kwa Pemba. Hata hivyo ukaguzi wa awali wa miche ya mikarafuu iliyopandwa msimu wa masika 2012 inaonesha kukua vizuri na wakulima wanaendelea kuihudumia vyema miti hiyo.

Mhe. Spika, kuhusu shauri la sensa ya Mikarafuu Wizara imo katika matayarisho ya kazi hii. Aidha, kupitia Mradi wa Kutathmini Miti na Mimea (Woody biomass inventory) kazi hii ya sensa ya mikarafuu inatarajiwa kuanza hivi karibuni. Fedha za kufanyia kazi hii tayari zimeshapatikana na wataalam watakaosimamia na kuendeleza kazi hii wanatarajiwa kuwasili hapa nchini wakati wowote kuanzia hivi sasa na mara tu kazi itakapokamilika, ripoti yake itatolewa na wananchi watajulishwa.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Ahsante sana Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri sana ya Mhe. Naibu Waziri wa siku nyingi wa serikali hii nina maswali mawili tu madogo.

Wakulima wamekuwa wakitikia sana wito huu wa kuchuka miche lakini elimu yao ni ndogo juu ya utunzaji wa miche hii. Jee, ni lini serikali itawapa elimu hiyo.

La pili ni sababu gani zilizopelekea wananchi wa Mkoa wa Kusini wakapewa miche kidogo tena kidogo sana, huoni ni kuwanyima haki wakati wao unaweza kusema ni watu wa pili au wa tatu katika kuitikia wito huu wa kilimo.

Ni sababu zipi Mhe. Spika, zilizopita hata wananchi wa Mkoa wa Kusini kupewa miche kidogo sana.

Mhe. Naibu Waziri wa Kilimo na Maliasili: Mhe. Spika, naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi maswali mawili ya nyongeza kama hivi ifuatavyo.

Ninakubaliana na yeye kwamba tutakuza elimu ya ukulima wa mikarafuu kwa wananchi ili tuweze kupata karafuu kwa wingi zaidi katika nchi yetu. Hilo moja.

La pili anauliza kwa nini Kusini imepewa miche kidogo. Nadhani Mhe. Spika, ni makisio na kuitizama ardhi ya Wilaya ya Kusini ilivyo. Eneo ambalo linalimika vizuri mikarafuu kwa Wilaya ya Kusini ni Muyuni kwa sababu pale ndio mikarafuu inaelekea kukubali.

Kwa hivyo miche imetoka kidogo lakini bado miche tunayo na angojee masika tu aje kuchukua miche mengine na tutawapa bila ya matatizo yoyote.

Mhe. Ali Abdalla Ali: Ahsante sana Mhe. Spika, na mimi kunipa fursa ya kuuliza swali la nyongeza pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri naomba nimuulize kama ifuatavyo.

Inasemekana kwamba miche ya mabotea ya mikarafuu inastahamili sana ukame kuliko miche hii inayokuwa kwenye vitalu. Jee, hilo ni kweli.

La pili kama ni kweli, jee wizara ina utaratibu gani wa kuhamasisha wananchi ili kutumia miche hiyo ili tuweze kupata mazao yaliyokuwa bora zaidi.

Mhe. Naibu Waziri wa Kilimo na Maliasili: Mhe. Spika, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake la nyongeza kama hivi ifuatavyo.

Mhe. Spika, suala alililoliuliza ni suala ambalo lipo wazi hata yeye akifikiri sana analipata jibu. Mabotea yanajitegemea na yanaishi katika mazingira magumu na yanastahimili mazingira magumu. Kwa hivyo imekuwa imeshazoea shida lakini kwenye kitalu pana raha, ukichukua miche kwenye kitalu imeshazoea raha ukaipeleka pahali ambako ichume wenyewe tatizo litakuwepo.

Kwa hivyo ndio tukasema katika taaluma waliyotolewa ni kufundishwa wananchi namna ya kuchimba yale mabotea vizuri zaidi ili yaweze kupatikana kwa wingi na ajue tu kwamba akitembea katika mashamba ya huko Mfenesini hivi sasa mabotea hakuna hata moja, kwa sababu wananchi wameyang'oa yote na wameyapanda yote.

Mhe. Mohamed Haji Khalid: Ahsante sana Mhe. Spika, na mimi nimuulize Mhe. Naibu Waziri swali moja dogo la nyongeza.

Kwa kuwa amekiri haya mabotea yenyewe yanastahamili zaidi ukame kuliko hii ya kitaalamu. Jee, wizara yako imefanya utafiti gani wa kuweza kuifanya hii ya kitaalamu nayo iweze kustahamili ukame.

Mhe. Naibu Waziri wa Kilimo na Maliasili: Mhe. Spika, naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake la nyongeza kama hivi ifuatavyo.

Mabotea huwa yanaota wenyewe kutokana na kubakia karafuu katika miti ya mikarafuu. Mhe. Mwakilishi karafuu zimepanda bei, mwaka huu hakuna botea, maana karafuu zote zimechumwa. Kwa hivyo hata tukiwaambia wananchi wangojee mabotea mwakani hawayapati, hiyo ndio hali halisi Mhe. Spika. Kwa hivyo itabidi waje wachukue kwenye vitalu. Ahsante sana.

HOJA ZA SERIKALI

Mswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria ya Usajili wa Mzanzibari Mkaazi Nam. 7 ya 2005

(Kusomwa kwa mara ya Pili)

(Majadiliano yanaendelea)

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe jana tulifikia pahala kumaliza michango, kwa hivyo leo moja kwa moja, naomba nimkaribishe Mhe. Waziri wa Nchi (OR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi.

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi: Mhe. Spika, nakushukuru sana kwa mara nyengine tena kunipa fursa hii kuja kufanya majumuisho ya michango mbali mbali ya Waheshimiwa Wajumbe kama walivyochangia katika mswada wetu huu wa marekebisho ya Sheria Nam. 7 ya mwaka 2005 ya Afisi ya Usajili na Kadi za Utambulisho Zanzibar.

Mhe. Spika, kwa kweli tunawashukuru sana Waheshimiwa Wajumbe wote waliopata fursa ya kuchangia hapa ukumbini na wale waliochangia kimaandishi. Najua kulikuwa na hamasa nyingi, michango mingi na kila mchango kwa kweli nathubutu kusema ulikuwa na haki ya kusema hivyo, kwa sababu kwa njia moja au nyengine wameyaona, wameyasikia lakini labda walikuwa pengine ule utaratibu kwa ukamilifu labda hawajaufahamu vizuri.

Sasa mimi nasema kama serikali *concerns* walizozieleza zote tumezisikia na yale yanayohusu sheria mimi nitazidi kuyasisitiza na naomba sana Waheshimiwa tujitahidi tuwaelimishe watu wetu, sheria haina matatizo kabisa, lazima tuifahamu yanayopaswa yafanywe na kama kuna kasoro za kiutendaji hizo mimi nitajitahidi nitakaa na wenzangu tuone kwamba tunazirekebisha vipi.

Naomba niseme kwamba juzi tarehe 28 mwezi uliopita tulikuwa Pemba na semina kubwa sana tuliwahusisha Masheha wote, Madiwani, Wakuu wa Wilaya na Wakuu wa Wilaya na Mikoa ya Pemba, na tumeshafanya semina kama hiyo Unguja.

Moja ya mada ilikuwa ni ya vitambulisho. Mkurugenzi wetu wa Vitambulisho alitoa mada na ilichangiwa vizuri sana. Mwanzo walijiorodhesha watu wengi sana kuchangia lakini baada ya maelezo wenyewe waliridhika kwamba kwa kweli hakuna matatizo kwenye sheria.

Tatizo ni kutokufahamu ile sheria yenyewe inataka vipi na kuifuata. Kuna watu wanataka kupita njia ya mkato ndio matatizo yote yapo hapo. Sasa Mhe. Spika, mimi ninapongeza sana michango ya Waheshimiwa Wajumbe na wamezungumza kwa hamasa rafiki yangu Mhe. Subeit Khamis Faki, Mhe. Saleh Nassor Juma, Mhe. Hija Hassan Hija, Mhe. Ali naye amezungumza na wengineo kwa kutetea hoja na ukweli wa mambo.

Kwa jumla Mhe. Spika, kulikuwa na michango 27 waliochangia; wawili walichangia kimaandishi na 25 walichangia hapa ukumbini. Naomba sasa niwataje wote mmoja baada ya mwengine.

1. Mhe. Mwenyekiti wa Kamati Mhe. Hamza Hassan Juma
2. Mhe. Mohamed Haji Khalid
3. Mhe. Hassan Hamad Omar
4. Mhe. Ussi Jecha Simai
5. Mhe. Asaa Othman Hamad
6. Mhe. Salum Abdalla Hamad
7. Mhe. Saleh Nassor Juma
8. Mhe. Ali Salum Haji
9. Mhe. Omar Ali Shehe
10. Mhe. Panya Ali Abdalla
11. Mhe. Suleiman Hemed Khamis
12. Mhe. Rufai Said Rufai
13. Mhe. Nassor Salum Ali
14. Mhe. Fatma Mbarouk Said
15. Mhe. Bikame Yussuf Hamad
16. Mhe. Makame Mshimba Mbarouk
17. Mhe. Marina Joel Thomas
18. Mhe. Farida Amour Mohamed
19. Mhe. Subeit Khamis Faki
20. Mhe. Mussa Ali Hassan
21. Mhe. Hija Hassan Hija
22. Mhe. Amina Iddi Mabrouk
23. Mhe. Salma Mussa Bilali
24. Mhe. Mahmoud Muhamed Mussa
25. Mhe. Machano Othman Said

Hao ndio waliopata fursa ya kuchangia hapa ukumbini.

Wale waliochangia kimaandishi ni Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi na yeye pia ni Makamo Mwenyekiti wa Kamati hii ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu na Mhe. Asha Abdu Haji.

Mhe. Spika, kama nilivyosema kwa kweli tunawashukuru sana kwa michango yao na ushauri wao, maelekezo yao yote waliyotupa sisi kwa upande wetu tutajitahidi kama watendaji ambao tunalisimamia suala hili kuona tunalifanikisha liende vizuri siku hadi siku.

Sasa kuna Wajumbe ambao naomba niwapongeze wale waliochangia na kuunga mkono hoja hii moja kwa moja ninawashukuru sana Wajumbe hao. (*Makofi*).

Lakini pia kuna Wajumbe pia naomba niwapongeze wale waliosema wataunga mkono baada ya marekebisho, wameuchambua mswada tunashukuru kwa vipengele tutajaribu kuvisoma au kurekebisha pale kama walivyouliza. Lakini kwa bahati mbaya ninasema wengi wetu hatukuenda kwenye mswada mara moja, yaani moja kwa moja kidogo tumechangia kwenye ile sheria mama na mambo mambo ambayo hatukuyaleta hapa.

Sasa yale mambo ambayo hatukuyaleta hapa ambayo wao wameyagusa tutakuwa kiukweli muda huu ni mdogo kuyaelezea yale mengine. Sasa hayo kwa kweli sio pahala pake, mimi nitazidi zaidi kugusa kwenye mswada.

Mhe. Spika, kama nilivyosema kuna wale waliokataa mswada kwa sababu wanahisi mswada mama urekebishwe kwa kulegeza masharti ambayo wanaona ni magumu. Kwa kweli Mhe. Spika, naomba kusema kwamba ni Waheshimiwa wa Baraza hili ambao mumekuwa mukieleza sana serikali, tukitwambia kila siku jamani wageni wanaingia kiholela nchini, uovu umezidi hawa watu hatuwatambui, wengine mpaka mukasema turejeshe pasipoti.

Lakini Mhe. Spika, tukasema aah! *Passport* itakuwa kwa wageni lakini kwa wengine hata hao wenzetu Wazanzibari waliopo nje wanataka kurudi wao bado wana *Passport* za Kitanzania. Sasa wale nao wameekea utaratibu wakitaka kurudi wafanye nini.

Sasa kulegeza masharti haya jamani itakuwa ndio tunaiachia nchi yetu wazi kabisa na hiki ni kisiwa na tunalalamika siku zote ajira hizi zetu nafasi wanapewa wageni. Sasa naomba niwarejeshe kwenye madhumuni makuu ya mswada huu na niliyasoma yale madhumuni lakini naomba niyakariri tena.

Madhumuni ya waraka huu ni kuifanyia marekebisho sheria Nam. 7 ya mwaka 2005 ili kutoa uwezo kwa Afisi ya Usajili na Utoaji Vitambulisho Zanzibar kufanya usajili na utoaji vitambulisho kwa wageni wanaoishi Zanzibar. Hatua hii itasaidia kisheria kukusanya taarifa binafsi za wageni na kuhifadhiwa katika mtandao ulio salama pamoja kuruhusu uchukuaji wa alama za vidole kwa wote watakaosajiliwa. Hayo ndio madhumuni makuu na nikatoa sababu kama 11 ku-*support* hoja hii, kwa nini tufanye hivyo. Sipendi kuzirejea nafikiri *Hansard* ipo mtu kama anataka kuzifahamu zaidi naomba azipitie.

Sasa Mhe. Spika, naomba niende kuchambua michango ya Waheshimiwa mmoja baada ya mwengine. Si mingi lakini kidogo ni mizito na ninahitaji niichambue mmoja baada ya mwengine. Wale wengine ambao kwa bahati mbaya sitowagusa nitawaomba radhi lakini nichukulie tu kwamba hoja zao tumezichukua na tutazifanyia kazi.

Naomba nianze na Mhe. Mwenyekiti wa Kamati; Mhe. Hamza Hassan Juma. Mhe. Mwenyekiti alituuliza au alishauri kwamba kifungu 6 (a) (3) (a) kijumuishe wafanyakazi wasio na mkataba kwa maandishi ambao pia wanatambulika kisheria.

Mhe. Spika, kuhusu kuongezewa sifa wa kutokuwa na mkataba wa kimaandishi, jibu lake linapatikana katika kifungu cha 6 (a) (3) (c) hapa utapata jawabu ya ushauri huo aliyotueleza au kutushauri Mhe. Hamza. Kifungu hicho kinaeleza kwamba mtu anayefanya kazi chini ya masharti au vigezo mbali mbali sambamba na vile vilivyoorodheshwa kwenye aya (a) na (b). Ukivisoma vyote kwa pamoja (a), (b) na (c) utapata jawabu la ushauri ule aliotoa Mhe. Hamza.

Hoja nyengine alishauri kwamba kuwepo kwa orodha ya masharti na vigezo kwa wafanyakazi ambao watapatiwa vitambulisho hivyo. Tunakubali kwamba suala la masharti ya wafanyakazi wanaostahiki kupatiwa vitambulisho limeshaelezwa katika mswada na masharti mengine, yatatokana na sheria zinazohusi taasisi husika kama Afisi ya Uhamiaji, Kamisheni ya Kazi na taasisi zinazosimamia uwekezaji kama ZIPA.

Naomba kusisitiza kwamba masuala ya uhamiaji, Kamisheni ya Kazi au ZIPA, wao wana jukumu lao na hatuingilii mamlaka zao, hatugusi mamlaka zao. Wao watakuwa wanaendelea na utoaji wa ruhusa zao. Sisi tunawasajili na kuwaona kwamba baada ya kupita huko tujue na huku wanafanya kazi gani, wanakaa wapi, wanakwenda mwenendo gani.

Nitatoa mfano Uswiss, tumeshafika Geneva mara nyingi tu nilipokuwa Wizara ya Afya, pale unaingia tu mgeni basi ukitokea *Airport* umeshamulikwa umeshajulikana unalala wapi, unakwenda wapi kila kitu *security* namna inavyokua, na sio wao tu ni nchi nyingi sana. Lakini Geneva Waswis wakali sana, wewe mwenyewe hujijui, lakini tokea unaingia basi unamurikwa kwa kila mwenendo wako, sasa sisi hatujafikia huko, lakini angalau tuwajue, wanafanya nini, wanalala wapi. Tunasema kwamba kuna wahalifu, kweli wengine wanatoka nje, lakini wengine tunao humu humu na wala hawajajisajili na wala hawana vitambulisho. Lakini wenetu humu humu hao waliozungumzwa Ubaya Ubaya, wengine wala sio wageni ni vijana wetu humu humu. Sasa na hawa nao tuwafahamu wanachanganyikana na hao wageni wanajificha kwenye mwamvuli wao.

Mhe. Spika, hoja nyengine Mhe. Hamza Hassan Juma alishauri kwamba kuwepo na adhabu kwa muajiri atakayekwenda kinyume na sheria hii. Kwa kumjibu Mhe. Hamza Hassan kwamba tunashauri katika sheria mama kuna orodha ya makosa na adhabu ambayo imeelezwa kwa kina, kwa yeyote asiyejisajili anayemsaidia mtu kujisajili kinyume na sheria na anayemshawishi muhusika kutojisajili pamoja na kutoa taarifa za uongo, akiwemo na muajiri kama ambavyo marekebisho yalivyoongeza kifungu 6A katika kifungu cha 14.

Hoja nyengine ya Mhe. Mwenyekiti, alitaka kushauri au alitaka kusema kwamba sheria iwatambue wakaazi wasio Wazanzibari ambao ni wanafunzi wanaotoka nje ya nchi. Mhe. Spika, kama ilivyo katika mswada ni kwamba tunakusudia kuwasajili wakaazi wote wasiokuwa Wazanzibari Wakaazi ambao ni mwenye kufuata masharti ya kiuhamiaji na usiokuwa na sharti la kufuata sheria za uhamiaji. Hivyo, wanafunzi wataingia katika makundi hayo.

Sasa kwa wale waliokuwa chini ya miaka 18 ni kweli marekebisho hayakuzingatia wageni waliokuwa chini ya umri wa miaka 18. Kwa hivyo, ushauri huu alioutoa Mhe. Mwenyekiti, tumeusikia, tunaukubali na tutauzingatia kwa kuufanyia kazi Mhe. Spika.

Pia alishauri kuwa vitambulisho viwe na rangi tofauti. Nafikiri vitambulisho tumevipitisha na tumeviona. Nilitaka kusema tu kwamba vitambulisho vinavyokusudiwa kutolewa vitakuwa na rangi na muonekano tofauti na vitambulisho tulivyovizowea vya Mzanzibari Mkaazi.

Mhe. Spika, Mhe. Hamza Hassan pia alishauri kwamba kiongezwe kifungu cha kuwapatia *DIASPORA* vitambulisho. Ninachotaka kusema ni kwamba suala la kuwapatia *DIASPORA* vitambulisho, sio vyema vikaingizwa katika sheria, kwani dhamira ya sheria hii ni kwa ajili ya wakaazi tu, nje ya utaratibu wa sheria hii basi Ofisi ya Usajili na Kazi za Utambulisho, inayo uwezo wa kutengeneza vitambulisho vya aina nyengine zozote iwapo itatakiwa kufanya hivyo, kama ambavyo tumeona katika aina ya vitambulisho vya namna mbali mbali tulivyovipitisha mbele yenu. Iwapo Idara ya *DIASPORA* wataona ipo haja ya kutengeneza vitambulisho, basi watawasilisha maombi yao katika ofisi ya vitambulisho.

Mhe. Spika, mchangiaji mwengine alikuwa ni mwanakamati Mhe. Mohamed Haji Khalid wa Mtambile. Lakini pia naomba nijumuishe na baadhi ya michango ya Mhe. Salim Abdalla Hamad wa Mtambwe, hawa kidogo mambo yao yanalingana. Kuhusu suala la tafsiri ya Mzanzibari kwa kujiandikisha.

Jibu lake tafsiri ya nani Mzanzibari imeelezwa katika ufasaha katika sheria nambari 5 ya mwaka 1985 na masharti ya kujisajili pia yameelezwa katika sheria nambari 7 ya mwaka 2005 pamoja na kanuni zake. Sasa alieleza kwamba masharti magumu ya kusajiliwa ikiwemo vyeti vya kuzaliwa, kwa hivyo nahisi kidogo tuyalegeze.

Mhe. Spika, jibu letu ni kwamba kwa muono wetu ni kwamba usajili hauna masharti magumu, ni kutambuliwa kwa Sheha na kuwa na cheti cha kuzaliwa. Mambo ambayo yote ni ya lazima kwa mujibu wa sheria za nchi hii, haya ni ya lazima jamani, hatuwezi tukawaachia watu waingie kiholela tu. Sasa ikiwa Sheha mnahisi yuko *bias*; katika semina yetu Pemba juzi, tulikubaliana kwamba Sheha yule ana jopo lake, yaani ana wajumbe 10 Sheha. Kwa hivyo, wale Wajumbe wamsaidie. Suala hilo tumetoa azimio kwenye semina yetu, viongozi wetu wakuu wote walikuwepo pale na hilo ni moja kati ya maazimio yetu. Sasa kuregeza hapo kwamba Sheha asiwe na mamlaka haiwezekani kwa mujibu wa sheria hii. Sheria zenyewe ambazo zimempa uwezo huyo Sheha na sheria nambari 1 ya mwaka 1998 ya tawala za mikoa na sheria ya vizazi na vifo nambari 10 ya mwaka 2006. Hizo ndio sheria ziliopo zinazomuwezesha huyu Sheha kufanya hayo. Sasa hayo anayosema sio sehemu ya mswada, wala sio maombi niliyoyaleta kwenye mswada. Lakini kwa vile mmeniuliza basi naomba nitoe taaluma ili tuzidi kuyafahamu.

Vile vile kulikuwa na suala la tafsiri ya neno 'Mzanzibari' kwamba ni tatizo na masharti yake yanakiukwa sana hususan kwenye cheti cha kuzaliwa. Hoja kwa nini kitambulisho hiki kimeandikwa kitambulisho cha Mzanzibari na si Mzanzibari Mkaazi. Mhe. Spika, sharti mama la mtu kuweza kusajiliwa na kupata kitambulisho ni kwamba muombaji ni lazima awe Mzanzibari. Hata hivyo, kwa kuwa kusajiliwa na kupatiwa kitambulisho ni jambo la lazima kisheria. *Is not a privilege* Mhe. Suleiman Hemed Khamis, uliuliza *is it a right or privilege*. Nasema ni la lazima kama Mzanzibari uwe nacho. Kama tulivyosema fursa nyingi kama benki na kadhalika kama tulivyosema hata ukikata tiketi uwe na hicho kitambulisho.

Kwa hivyo, huo ni ukweli kabisa, hili ni shuruti letu sheria tuliyoipitisha kila Mzanzibari awe nacho. Ili kuhakikisha sheria hii inatekelezeka ndipo likawekwa sharti kwamba muombaji lazima awe na makaazi ya kudumu hapa Zanzibar, huyo ndio Mzanzibari Mkaazi. Kwani Wazanzibari ambao wapo nje ya Zanzibar, iwapo utawawekea sharti la lazima wawe na vitambulisho, basi utekelezaji wa sheria hii utakuwa mgumu, ama ingewalazimu warejee nchini kwa kujisajili vyenginevyo wangepoteza Uzanzibari wao. Au serikali ingelazimika kufungua ofisi duniani kote. *Alhamdullilah* Wazanzibari wapo ulimwengu mzima, sasa tupite huko tukawaandikishe au tuwaite warudi hapa, kwa kweli wazungu wanasema *is not practicable*. Utekelezaji wake ni mgumu, haliwezekani hilo.

Ndio tukaweka sasa ili kuhakikisha kwamba Wazanzibari walioko nje hawapotezi haki ya kupewa kitambulisho, katika sheria mama kifungu cha 8 kinamtaka Mzanzibari aliyekuwa nje ya nchi, mara tu atakaporudi nchini ndani ya mwezi mmoja anawajibika kujisajili na kupewa kitambulisho chake, ilimradi tu awe hajapoteza uraia wake wa Tanzania. Kwa hivyo, tumeweka nafasi hiyo kwa hao Wazanzibari walioko nje watakaporudi waweze kusajiliwa, kwa hivyo nafasi ipo hatuwafukuzi wala hatuwakatazi.

Mhe. Spika, rafiki yangu Mhe. Mohamed aliuliza kuwa yeye ni mkaazi wa Kengeja je anaweza kuchukua ukaazi wa Chukwani. Najua anaishi Chukwani Mhe. Mohamed ndio maana akauliza hivyo. Ukweli ni kwamba kwa mujibu wa katiba Mzanzibari huyo kwenye kifungu cha 16 kimeelezwa kuwa anao uwezo wa kuishi popote Zanzibar, hakuna mipaka. Lakini utaratibu wa kuhama kutoka sehemu moja kwenda sehemu nyengine, mwananchi anatakiwa kuchukua barua kutoka Shehia anayohama na kuiwasilisha kwa Sheha wa Shehia anayohamia na baada ya hapo atapatiwa barua itakayomuwezesha kwenda kubadili taarifa za kitambulisho chake katika kituo cha Wilaya anapohamia. Sasa matatizo yako hapa. Watu wetu wengi hawayafanyi haya, wanahama na kuhamia freely, sawa inakubalika aende tu. Lakini kwanza anakotoka achukuwe barua na kule akifika aripoti ili aweze kusajiliwa. Sasa wengi wa watu wetu hawayafanyi haya.

Mhe. Spika, mchangiaji mwengine alikuwa Mhe. Asaa Othman Hamad, ambaye alizungumza kwa hamasa kweli kweli na *concern* yake kwa wale wanaoitwa ubaya ubaya. Sisi kama serikali tumesikia na kwa kweli hali ni mbaya na tutajipanga ili tuone tunafanya nini. Kama nilivyosema na hawa wengine tunawafikiria ni wageni wengine sio wageni ni vijana wetu humu humu, wanafuata mkumbo tu wanavuta bangi na madawa ya kulevya na kutafuta mbinu za kujipatia mapato bila ya kufanyakazi. Kwa hivyo, *concern* yako tumeisikia kweli, usalama wa watu wetu au wananchi wetu umekuwa mdogo na unatishia amani. Kwa hivyo, hili tumelisikia kama serikali na tutajipanga ili tuone tunafanya nini.

Mimi jana nilizungumza na Kamishna wa Polisi usiku baada ya kusikia mfanyakazi wangu mmoja wa Ikulu gari yake nayo imepigwa panga. Kataka kusimamishwa akakataa basi panga likarushwa na likavunja kiyoo. Kwa hivyo, haya mambo kweli yapo na yanatisha Mhe Asaa Othman na tumesikia, hilo tutalifanyia kazi.

Pia aliuliza kwamba wasiostahiki na vitambulisho vya Mzanzibari Mkaazi ndio wanaopewa. Kuna wimbi kubwa la uhalifu wamepewa vyeti vya kuzaliwa na wamepewa vitambulisho. Jibu, kwa kuwasajili wageni na kuwapatia vitambulisho kuna lengo la kupunguza kiu na haja ya kutafuta vitambulisho vya Mzanzibari Mkaazi. Hii ni imani yetu kwamba itapunguza watu wasiostahiki kujisajili kinyume na sheria. Baadae nitaunganisha na Mhe. Hija Hassan ambaye aliuliza kama wako watu ambao tumewatia hatiani.

Mhe. Salim Abdalla wa Mtambwe alituuliza kwamba *directive of the minister* tunakusudia nini na alihisi yeye kwa mtizamo wake ni kwa sababu ya watu kutoa kitambulisho, kuwa waziri anatoa maagizo nje ya utaratibu. Hii kwa kweli si sahihi Mhe. Mjumbe najua unafahamu, lakini unataka labda ufafanuzi zaidi tu. Pale kauli iyosemwa sio kauli hasa, lakini kilichokusudiwa ni kwamba kifungu nambari 13 kinampa uwezo Waziri kupokea rufaa na hivyo hivyo inampa uwezo waziri kutoa maelekezo kwa Mkurugenzi ambapo maelekezo yenyewe hayatokwenda kinyume

na sheria. Zile *directives* zenyewe ni tatu, nafikiri ukizisoma utaziona moja, mbili na tatu. Kwa hivyo, Waziri hatotoa maagizo au maelekezo nje ya *directives* zile pale zilizoorodheshwa.

Hoja nyengine uliuliza kwamba Mkaazi asiyekuwa Mzanzibari ameingia kutoka wapi. Naomba nikujulishe kwamba Mkaazi asiyekuwa Mzanzibari ni mgeni yeyote aliyeingia kihalali kutoka mahali popote duniani.

Halafu akauliza tena Mkaazi wa muda ni yupi. Maana ya Mkaazi wa muda umeshaelezwa wazi katika mswada kifungu cha 3(e) ukifungua pale nafikiri utaona. Mkaazi wa muda imeelezwa kwa wazi kabisa Mheshimiwa.

Hoja nyengine amesema kwa nini anayepaswa kusajiliwa akae hadi muda ulioainishwa katika sheria hii. Jibu lako ni kwamba kwa vile ni jambo la lazima kisheria mswada umetoa muda wa kutosha ili kuwapa fursa kwa wahusika kuweza kujisajili, tumetoa muda mzuri kabisa yeye ajiandae kusajiliwa ili kusiwe na bughdha.

Mhe. Ali Salum Haji wa Kwahani tunakushukuru sana Mheshimiwa kwa ufafanuzi wako wa kuondoa hizi stafahamu za ukabila na udini kwa kweli hayo hayatusaidii. Tumeamua mambo haya tusiyalete nchini mwetu kuuliza huyu anatokea Mtwara, huyu anatokea Mtambwe. Hayo hayatusaidii sote ni Wazanzibari, sote nia yetu ni moja, na sasa tuko pamoja zaidi kuliko huko nyuma. Haipendezi tena kurudi tukaanza kutafutana, huyu anatokea wapi na anakwenda wapi. Kwa hivyo, mimi nakushukuru sana Mhe. Ali Salum Haji kwa ufafanuzi wako mzuri kabisa ambao umekemea suala hili la ukabila kulirejesha nchini mwetu.

Mhe. Omar Ali Shehe na wewe nakushukuru sana kwa mchango wako na uliuliza kwamba Wazanzibari wenyewe wamekuwa na malalamiko na wamenyimwa fursa. Sio kweli Mhe. Omar Ali baadae nitatoa takwimu hapa utazisikia. Mtu yeyote ambaye ana sifa za kusajiliwa basi anasajiliwa kwa mujibu wa sifa zilizoainishwa katika sheria nambari 7 ya mwaka 2005 na sheria nambari 5 ya mwaka 1985, pamoja na sheria ya vizazi na vifo nilizozitaja nambari 10 ya mwaka 2006 na sheria nambari 1 ya mwaka 1998 ya tawala za mikoa. Haya yote yanafanywa kwa mujibu wa sheria ziliopo nchini, hatuendi nje ya taratibu za kisheria.

Mhe. Suleiman Hemed na Mhe. Salim Abdalla, kuna mambo ambayo mliuliza kwa pamoja. Kwanza ni suala la *biometric information*. Sheria mama Mhe. Spika, ilikuwa inamtaka mwananchi kuchukuliwa alama za vidole gumba peke yake, wakati mabadiliko ya teknolojia hivi sasa inahitajika kuchukua alama za vidole vyote na ikilazimu alama nyengine za kibayolojia kama vile mboni ya jicho, DNA na kadhalika. Hiyo ndio maana halisi ya taarifa ya ki-*biometric*. Hata ukisoma kwenye ufafanuzi pale imeelezwa kwa uwazi kabisa, nafikiri kwenye sehemu ya pili, marekebisho ya kifungu cha 3A imeeleza maana ya ki-*biometric*.

Mhe. Spika, hoja kuhusu shughuli zisizokuwa na leseni. Mhe. Spika, sheria haikubagua wafanyabiashara waliokuwa na leseni na wasiokuwa na leseni, kwa sababu hii tumeifanya kwa makusudi, kwani wote wanahusika na sheria hii. Aidha, kwa kufanya hivyo tutaweza kuwabaini wafanyabiashara zisizo rasmi na hawana leseni na wapo wengi tu. Kwa hivyo, hii tutawasaidia mamlaka nyengine katika kuwabaini hao wanaiongia nchini na hawana leseni. Kwa hivyo, hii pia itasaidia kuwakamata hao wanaofanya biashara wanaohalifu sheria na wasiokuwa na leseni. Yaani wale wasiokuwa na leseni na wenye leseni, kwa hivyo, sheria hii nayo itasaidia sana.

Mhe. Suleiman Hemed ipa alitaka kujua tafsiri ya Mzanzibari Mkaazi, asiyekuwa Mzanzibari Mkaazi, Mkaazi wa Muda na kuwe na uraia. Hayo mambo mawili nafikiri nimeshayazungumza. Lakini nataka kusema kwamba Zanzibar ilipoungana na Tanganyika mwaka 1964, tulikubaliana kwamba suala la uraia liwe suala la Muungano. Kwa hivyo, uraia wetu ni wa Tanzania, hakuna uraia wa Unguja Mhe. Suleiman, hakuna uraia wa Unguja tena kwa mujibu wa katiba iliopo. Tukitaka kurekebisha hilo, basi ni lazima turudi katika Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Sasa hivi kuna fursa ya kutoa maoni, toa maoni yako kwamba turekebishe uraia uwe hivi. Lakini sisi kwa mujibu wa sheria hii hatuwezi kufanya hivyo.

Mhe. Spika, pia Mhe. Suleiman Hemed alitoa hoja yake kwamba Wazanzibari kupewa kitambulisho ni haki au *privilege*. Nafikiri nimezungumza kwamba kuwa na kitambulisho ni haki na wajibu wa kila Mzanzibari mwenye sifa, hili naomba kusisitiza sana. Ni wajibu kwa kila Mzanzibari mwenye sifa, kama ilivyoainishwa katika sheria nambari 7 ya mwaka 2005 iliyopitishwa na Baraza lako tukufu.

Mhe. Spika, Mhe. Rufai Said Rufai na Mhe. Hassan Hamad Omar, Mhe. Farida Amour Mohamed na Mhe. Subeit Khamis Faki kwa pamoja, naomba nijibu hoja moja ambayo waliuliza kwamba Mheshimiwa ulituahidi mwezi wa saba hapa kuwa tutafanya ziara na tutakwenda huko *field*, Mheshimiwa mbona kimpya mpaka leo.

Waheshimiwa Wajumbe, tumeanza utekelezaji wa hiyo ahadi yangu, lakini tumeanza vyengine kwanza. Tulihisi kulikuwa na semina ilishafanywa Unguja kama nilivyosema ya Masheha, Madiwani, Wakuu wa Mikoa na Wakuu wa Wilaya. Halafu tulikwishapanga semina kama hiyo tukaifanye Pemba, na moja ya mada ilikuwa ni suala la vitambulisho. Sasa tulihisi kwanza acha hawa watendaji wote, madiwani, masheha na wengine, wapate dozi kidogo ya hii sheria. Kwa hivyo, sasa hivi *Alhamdulillah* mkutano ulifanyika mzuri kabisa, tulipata *interaction* vizuri kabisa, waliuliza maswali yao wakajibiwa. Sasa hivi mimi niko tayari Waheshimiwa Wajumbe tupange ili twendeni *field*, lakini tupange vizuri, kwa sababu shughuli zinapishana. Mimi nikija Pemba nyinyi mnakuja kwenye Kamati, lakini tutapanga kidogo kidogo. Ndio kwanza mwezi wa nne huu au wa tatu tokea mwezi Julai. Kwa hivyo, bado tunayo nafasi kabla ya bajeti nyengine tuje tupange ili tuone tutafikia wapi.

Lakini nataka kusema kwamba kwa upande wa Unguja, tunamshukuru sana Mhe. Makame Mshimba Mbarouk, ambaye yeye mwenyewe alihimiza na tukashirikiana kufanya kazi hiyo kwa upande wa Unguja. Tumeanza kidogo na yeye anatupa *query* nyingi, tukienda kwake na kazi imeanza kwa kiwango fulani tunashkuru. Kwa hivyo, dhamira tunayo tusiwe na wasi wasi tutapanga na tutakuja *field* tuone haya matatizo yakoje na tuyarekebishe vipi. Jambo la kufurahisha ni kwamba tulipokuwa semina ya Pemba, Waheshimiwa Madiwani na Waheshimwia Masheha waliuliza maswali na wakapata majibu pale pale, mpaka wenyewe wakaona kumbe tatizo liko kwetu sisi wenyewe tu hatusimamii sheria ipasavyo. Mwanzo walikuwa na maswali zaidi ya 50, lakini walijiorodhesha, baada ya kujibiwa wanne tu wameridhika kabisa.

Kwa hivyo, nataka kusema haya masuala mengi labda ni kutofahamu tu na wengine kutaka *shortcut.* Lakini baya zaidi ambalo baadae nitakuja kulisema ni *forgery*, kuna watu wetu wengi sasa hivi wanafanya *forgery*, hasa katika vyeti vya kuzaliwa na hao wameshabainika, na suala la *forgery* hapa kwetu sasa limeshakuwa kubwa, vyeti vya skuli na mambo mengi yanayohusu vyeti watu siku hizi ku-*forge* imekuwa ni jambo la kawaida.

Kwa hivyo, Waheshimiwa Wajumbe nawaombeni sana, sisi ndio wenye wananchi hivyo tuwasimamieni, vijana wetu wana-*forge* vyeti wengi sana, hasa vya skuli. Anakwenda kule labda kwenye *interview* anapeleka cheti, kisha baadae inakuja kujulikana kumbe cheti ka-*forge.* Sasa haya mambo ndio yote tuyapigeni vita.

Mhe. Spika, Mhe. Hija Hassan Hija na yeye alikuwa na mengi madogo madogo ya kuuliza na aliniambia kwamba hakubaliani kuwa usajili umefanikiwa. Mimi nataka kumuhakikishia Mhe. Hija Hassan kwamba usajili umefanikiwa kweli kweli. Naomba uchukue karatasi sasa nikupe takwimu za usajili mpaka tarehe ya leo tarehe 17/10/2012, nitakupa jimbo kwa jimbo. Naomba Mhe. Spika, uniachie muda kidogo ili nisome majimbo yote.

Mhe. Spika, nitakwenda kwa *alphabetical*.

1.	Jimbo la Amani, waliosajiliwa watu	12,345
2.	Jimbo la Bububu waliosajiliwa watu	14,149
3.	Jimbo la Bumbwini waliosajiliwa watu	8,775
4.	Jimbo la Chaani waliosajiliwa watu	10,755
5.	Jimbo la Chache Chake waliosajiliwa watu	11,838
6.	Jimbo la Chambani waliosajiliwa watu	7,040
7.	Jimbo la Chonga waliosajiliwa watu	8,648
8.	Jimbo la Chumbuni waliosajiliwa watu	16,031
9.	Jimbo la Chwaka waliosajiliwa watu	12,829
10.	Jimbo la Dimani waliosajiliwa watu	19,588
11.	Jimbo la Dole waliosajiliwa watu	11,923
12.	Jimbo la Donge waliosajiliwa watu	13,349
13.	Jimbo la Fuoni waliosajiliwa watu	15,620
14.	Jimbo la Gando waliosajiliwa watu	9,292
15.	Jimbo la Jang'ombe waliosajiliwa watu	14,074
16.	Jimbo la Kiembesamaki waliosajiliwa watu	8,161
17.	Jimbo la Kikwajuni waliosajiliwa watu	13,159
18.	Jimbo la Kitope waliosajiliwa watu	10,047

19. Jimbo la Kiwani waliosajiliwa watu 7,488
20. Jimbo la Koani waliosajiliwa watu 15,651
21. Jimbo la Kojani waliosajiliwa watu 9,968
22. Jimbo la Konde waliosajiliwa watu 9,773
23. Jimbo la Kwahani waliosajiliwa watu 12,153
24. Jimbo la Kwamtipura waliosajiliwa watu 15,640
25. Jimbo la Magogoni waliosajiliwa watu 14,428
26. Jimbo la Magomeni waliosajiliwa watu 15,902
27. Jimbo la Makunduchi waliosajiliwa watu 11,127
28. Jimbo la Matemwe waliosajiliwa watu 8,195
29. Jimbo la Mfenesini waliosajiliwa watu 10,037
30. Jimbo la Mgogoni waliosajiliwa watu 8,869
31. Jimbo la Micheweni waliosajiliwa watu 9,890
32. Jimbo la Mji Mkongwe waliosajiliwa watu 14,194
33. Jimbo la Mkanyageni waliosajiliwa watu 8,096
34. Jimbo la Mkoani waliosajiliwa watu 9,996
35. Jimbo la Mkwajuni waliosajiliwa watu 8,929
36. Jimbo la Mpendae waliosajiliwa watu 14,467
37. Jimbo la Mtambile waliosajiliwa watu 9,693
38. Jimbo la Mtambwe waliosajiliwa watu 8,506
39. Jimbo la Mtoni waliosajiliwa watu 14,238
40. Jimbo la Muyuni waliosajiliwa watu 0,421
41. Jimbo la Mwanakwerekwe waliosajiliwa watu 13,364
42. Jimbo la Nungwi waliosajiliwa watu 9,560
43. Jimbo la Ole waliosajiliwa watu 9,534
44. Jimbo la Rahaleo waliosajiliwa watu 12,355
45. Jimbo la Tumbatu waliosajiliwa watu 10,398
46. Jimbo la Tumbe waliosajiliwa watu 9,696
47. Jimbo la Uzini waliosajiliwa watu 11,797
48. Jimbo la Wawi waliosajiliwa watu 13,470
49. Jimbo la Wete waliosajiliwa watu 12,144
50. Jimbo la Ziwani waliosajiliwa watu 10,352

Mhe. Spika, jumla ya majimbo yote waliosajiliwa ni laki 577,954. Hii Mhe. Spika, inaonesha asilimia zaidi ya 100 ya makadirio yetu ya usajili. Sasa Mhe. Hija Hassan ukisema hatukufanikiwa

TAARIFA

Mhe. Spika: Taarifa Mhe. Suleimani Hemed Khamis.

Mhe. Suleiman Hemed Khamis: Mhe. Spika, Jimbo la Konde sikulisikia halikutajwa katika utaratibu huu. Naomba nilisikie.

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi: Jimbo la Konde Mhe. Suleiman Hemed waliosajiliwa ni watu 9,773.

Mhe. Spika, naomba kusisitiza tena, makadirio yetu ya usajili basi hii imepindukia asilimia 100. Kwa hivyo, mimi ninachotaka kusema zoezi hili limefanyika kwa uadilifu bila ya ubaguzi wowote Mhe. Nassor, hakuna ubaguzi. Kama kungekuwa na ubaguzi basi takwimu hizi usingezipata, haulizwi mtu itikadi ya chama chake, haulizwi kadi yake, wala haulizwi *affiliation* yake ya chama gani, usajili ushahidi ni huu hapa Mhe. Spika. Sasa mimi naomba sana Wajumbe tuwaelimishe watu ili wafahamu nini kinatakiwa na nini kisichotakiwa, hilo ndio suala la msingi kabisa.

Mhe. Hija Hassan Hija pia aliniuliza kuna kesi gani ambazo zimeshughulikiwa na ofisi hii. Nataka kumuambia kwamba kesi zilizofika ofisini ni 19, ambapo kesi 5 za Wazanzibari na 14 ni za wanaotuhumiwa kuwa ni wageni na ziko katika vyombo vya sheria.

Kwa bahati nzuri nyengine huwa hatuzibaini wenyewe, lakini wanapokwenda kwenye kuomba kazi au taratibu nyengine ndipo wanapobainika, ninayo orodha hapa na baadaye nadhani kwa ku-*save* muda nisiisome.

Lakini kuna raia wa Comoro, Kenya, Oman, Msumbiji na hao wote ndio katika hao niliosema kwamba kuna kesi hizo 19 kwa ujumla. Kwa mfano, kesi nyengine ziko Uhamiaji, nyengine ziko Polisi na nyengine Mahakamani ambazo ndio nyingi na wala hakuna ambayo imeachiliwa, na kila iliyobainika basi hatua za kuifuatilia zinachukuliwa.

Mhe. Spika, Mhe. Amina Iddi Mabrouk, Mhe. Salma Mussa Bilali, Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa, kwa kweli tunawashukuru kwa michango yao na hasa Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa kwa kuchambua historia ya Mzanzibari, yaani umetupatia lile chimbuko la pass vile ilivyoanza na tofauti ya wakati ule ya yule mkaazi vile ilivyotajwa wakati ule. Kwa hivyo, tunakushukuruni sana kwa michango yenu. *(Makofi)*

Mhe. Machano Othman Said (Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum) kwa mchango wake wa uchambuzi wa kina juu ya mswada huu, pamoja na ushauri aliotoa wa kusimamia vyema sheria hii.

Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi na Mhe. Asha Abdu Haji vile vile na nyinyi tunawashukuru kwa michango yenu mliyotupa, pamoja na ushauri wenu mliotupa tunaupokea.

Mhe. Spika, kabla sijaenda kwenye michango ya Waheshimiwa Wajumbe wengine naomba nitoe hoja kidogo nisije kusahau kwa ujumla.

Mhe. Spika, utafiti tulioufanya katika kitengo chetu na serikali kwa jumla umetudhihirishia kwamba hakuna malalamiko yaliyotokea kwenye sheria, isipokuwa masuala ya kiutendaji ndio ambayo yametufikia. Kwa hivyo, sisi serikali kama nilivyosema hatukatai na hayo tutayasimamia tutayafuata, lakini muhimu hao wanaolalamika sasa wafuate sheria kwamba sheria inasemaje.

Vile vile nataka kusisitiza kwamba kumekuwa na madai ya upotoshaji wa uhalisia wa jambo lenyewe na hilo ndilo kubwa ambalo limejitokeza. Hali hii inatokana na kwamba vigezo vinavyofanya tufikie maamuzi hayo ni kama ifuatavyo.

Mhe. Spika, kama nilivyosema hadi tarehe ya leo nimewataja wale watu 577,954 ambao tayari wameshasajiliwa na vitambulisho vimeshatengenezwa, hii ni idadi zaidi ya asilimia mia moja ya lengo la watu wote waliotarajiwa kusajiliwa.

Pia Sheria ya Usajili inatoa fursa kwa mtu yeyote mwenye sifa na akakataliwa kusajiliwa na kupewa kitambulisho anatakiwa kukata rufaa kwa Mkurugenzi, na iwapo hajaridhika na maamuzi ya Mkurugenzi pia anaweza kukata rufaa kwa Waziri husika.

Hata hivyo, Mhe. Spika kwa sasa katika Ofisi ya Mkurugenzi kuna rufaa nne tu, ambazo mbili ni Shehia ya Mtopepo na mbili Kwaalinatu, na mimi mwenyewe kama Waziri sijapokea rufaa hata moja bado sijaipata.

Mhe. Spika, hadi leo tarehe 17/10/2012 kuna jumla ya vitambulisho 112,420 vimelimbikizana katika vituo vya usajili na wenyewe hawajajitokeza kwenda kuvichukua.

Mhe. Spika: Mhe. Naibu Waziri wa Afya, nakusudia kumwambia usubiri kidogo.

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi: Mhe. Spika, mpaka leo vitambulisho 112,420, basi tunaomba wenyewe wajitokeze wakavichukue, pengine malalamiko haya yaliopo kwamba hatujapewa vitambulisho ndio hao wameshasajiliwa lakini hawataki kwenda kuvichukua.

Sasa naomba niisome tena kiwilaya. Wilaya ya Wete kuna vitambulisho Mhe. Asaa Othman Hamad kuna vitambulisho 9002 havijachukuliwa vipo, Micheweni Mhe. Subeit Khamis Faki kuna vitambulisho 6939 havijachukuliwa tusaidie, Wilaya ya Chake Chake Mhe. Omar Ali Shehe kuna vitambulisho 8242 tunakuomba

utusaidie wenyewe hao wakavichukue, Mkoani kuna vitambulisho 7059 Mhe. Abdalla Moh'd Ali bado havijachukuliwa vipo, na pengine watu ndio wanaolalamika kwamba tupewe vitambulisho ndio hivi wajitokeze.

Kwa upande wa Unguja Wilaya ya Mjini kuna vitambulisho 28,713 *Form VI* au Chuo Kikuu hapa, Magharibi kuna vitambulisho 22,193, Kati kuna vitambulisho 7579, Kusini kuna vitambulisho 2375, Kaskazini 'A' kuna vitambulisho 13,230, Kaskazini 'B' kuna vitambulisho 7088. Kwa hivyo, jumla yote Mhe. Spika vitambulisho ambavyo havijachukuliwa ni 112,420, *speed* yake imekuwa ni ndogo wanakwenda watu wawili au watatu na hii ndio *figure* tuliyonayo.

Sasa jamani tungekuwa na ubaguzi vitambulisho havitolewi na hivi vimeshaandikwa vipo wakavichukue wenyewe. Kwa hivyo, tunakuombeni sana Waheshimiwa Wajumbe mtusaidie na isiwe tumepoteza *resources* nyingi kuvitengeneza na watu walikwenda, lakini sasa hawaendi kuvichukua kwa kweli haifurahishi.

Kwa hivyo, nataka nikuhakikishieni tu kwamba kitengo chetu pamoja na serikali yetu kwa nia safi imelifanya hili zoezi kwa uadilifu mkubwa.

Mhe. Spika, naomba kuongezea kwamba utaratibu uliopo wa usajili hautoi mwanya wa ubaguzi wa kisiasa, kwani katika vielelezo vinavyohitajika, ili usajiliwe mwananchi kama nilivyosema haulizwi kadi yake ya chama chake cha siasa.

Hivyo, msajili hawezi kujua msimamo wa kisiasa wa muombaji na matokeo yake tumeyaona haya majimbo takriban ya Pemba yote yamechukuliwa na CUF na wala hakuulizwa mtu na vitambulisho wamepewa, na baadhi ya majimbo ya Unguja hivyo hivyo, na wala hakuulizwa mtu. Kwa maana hiyo, hakuna *affiliation* ya kisiasa hapa na ushahidi ndio huo. *(Makofi)*

Mhe. Spika, hali hii inathibitisha kwamba hakuna tatizo la upatikanaji wa kitambulisho, isipokuwa kilichopo ni upotoshaji wa ukweli wa mambo. Kwa kweli kiini cha upotoshaji huu ni ukweli kwamba idadi ya watu waliojiandikisha kupiga kura katika Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2005, naomba mnisikilize vizuri hapa, wananchi waliojiandikisha kupiga kura katika Uchuguzi Mkuu wa mwaka 2005 ilipungua kulingana na walioandikishwa kwa ajili hiyo mwaka 2000.

Kwa hivyo, hali hiyo iliwapa wasi wasi baadhi ya watu na wakatafuta jibu rahisi na kusingizia hali hiyo ilisababishwa na watu kutopewa vitambulisho. Lakini ukweli halisi ilisababishwa na udhibiti uliofanywa na Tume ya Uchaguzi katika kuzuia watu kujiandikisha zaidi ya mara moja, kuandikisha watoto wadogo na kuandikisha watu wanaotoka nje ya Zanzibar, na matokeo ndio haya *figure* niliyoisoma.

Kwa hiyo, matokeo ni kwamba kuna idadi kubwa ya vitambulisho ambavyo wenyewe hawajaenda kuvichukua, ndio hao niliowataja ambao wengi na wala hawapo hawa na huo ndio ukweli kabisa. Kutokana na hali hiyo, nakipongeza sana Kitengo chetu cha Usajili wa Mzanzibari Mkaazi kwa kufanya kazi nzuri sana. *(Makofi)*

Mhe. Spika, kwa bahati mbaya sana upotoshaji wa aina hii unaendelea kwa kuendelea kutoa kauli zile zile zilizotolewa mwaka 2005 bila ya kufanya utafiti wala kuzingatia mazingira halisi.

Kwa maana hiyo, natoa wito kwa viongozi wenzangu hasa sisi wanasiasa tutambue kwamba vitambulisho si *agenda* ya kisiasa, na kuna watu walizungumza kuwa ni *agenda* ya kisiasa, na wala sio *agenda* ya kisiasa na mfano tumeuona kwamba nimesoma kwa majimbo.

Kwa hivyo, nawaomba sana tushirikiane kuwaelimisha wananchi pia tusaidiane katika kuwahimiza wananchi kuheshimu na kufuata sheria za nchi badala ya sisi kuwapa misimamo ambayo kidogo inajenga chuki na hasama kati yetu na serikali yetu.

Mhe. Spika, naomba sasa nimalizie michango mingine ambayo ni michache tu iliyobaki. Lakini kwa ujumla nataka kusema kwamba naona nimemaliza. Kwa jumla kuna baadhi ya Waheshimiwa ambao walichangia jioni ya jana, ambao wengi wametuunga mkono masuala ambayo walituuliza na pia waliunga mkono mswada na nataka kusema kwamba yale ambayo wametuelekeza katika utendaji. Kwa kweli yote tumeyachukua na tutayafanyia kazi, na pale

binadamu ambapo mmoja au mwengine sikumjibu basi asione kama tumedharau, lakini ushauri tumeuchukua na tutaufanyia kazi.

Mhe. Spika, nawaomba sana Waheshimiwa Wajumbe kwamba tujaribu sana kuwaelimisha wananchi wetu suala zima la sheria, nafikiri kama kuna mapungufu ya sheria basi sisi ndio Wawakilishi ni vyema tushauri, tuzungumze na tuweze kuirekebisha. Lakini mambo ya msingi ya mswada huu tumeyafahamu nini madhumuni ya mswada huu.

Mhe. Spika, kwa hayo sasa naomba nichukue fursa hii kukushukuru sana pamoja na Waheshimiwa Wajumbe wote na naomba kutoa hoja.

Mhe. Waziri Afya: Mhe. Spika, naafiki.

Mhe. Spika: Mhe. Waziri, ahsante sana nadhani busara tumeiona kwamba shughuli hii jana tuliiakhirisha hadi leo hii, kwa ajili ya kupata wasaa na kutoa mambo mengi haya ambayo Mhe. Waziri ameyatoa. Nakushukuru sana Mhe. Waziri.

Kwa hivyo, sasa Waheshimiwa Wajumbe niwahoji wale wanaokubaliana na hoja ya mswada huu wanyanyue mikono, wanaokataa, waliokubali wameshinda. *(Makofi)*

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

Mhe. Waziri wa Nchi, (OR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi: Mhe. Spika, naomba kutoa taarifa kwamba Baraza lako tukufu likae kama Kamati ya Kutunga Sheria, ili kuupitia mswada wangu kifungu baada ya kifungu.

KAMATI YA KUTUNGA SHERIA

TAARIFA

Mhe. Omar Ali Shehe: Mhe. Mwenyekiti, naomba muongozo wako unisaidie kidogo, kuna madhumuni na sababu katika mswada huu, kwa bahati mbaya madhumuni na sababu haikuwekewa kifungu, na mimi nataka nihoji kitu ambacho kinahusiana na madhumuni na sababu. Mhe. Mwenyekiti, naomba unielekeze nifanye nini.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Mjumbe, sina hakika, lakini kama nakumbuka sawa sawa katika mambo yaliyotangulia mwanzo kabisa Mhe. Waziri kuyatolea, na akasema kuna sababu 11 ilikuwa anakwenda kwenye sehemu hiyo baada ya madhumuni na sababu.

Vile vile hii ni kitu kilichopelekea haja mpaka kufikia kutengeneza mswada huu, lakini haiingii kuwa ni sehemu ya mswada ni kama maelezo tu yale ambayo yameifanya serikali ifikie pahala na iseme tunatengeneza mswada huu kwa sababu moja, mbili, tatu, nne, tano lakini si sehemu ya mswada.

Kwa maarifa tuliyonayo hapa pamoja na wewe mwenyewe Mhe. Mjumbe, wakati tunapopitisha vifungu wala huku kwenye madhumuni hakuna kifungu chochote tunachokipitisha, nadhani huo ndio utaratibu wa muda wote. Kwa hivyo, isipokuwa haya ni maelezo yaliyopelekea serikali kufikia pahala ikaona umuhimu na haja ya kutengeneza mswada huu. Nafikiri tuendelee.

Mswada wa Sheria ya Usajili wa Mzanzibari
Mkaazi (Marekebisho) ya 2012

Sehemu ya Kwanza
Utangulizi

Kifungu 1 – Jina fupi na kuanza kutumika.
Kifungu 2

Mhe. Suleiman Hemed Khamis: Mhe. Mwenyekiti, wakati nilipokuwa nikichangia jana nilimtaka Mhe. Waziri atoe tafsiri ya neno mkaazi, na kwa sababu hichi kitambulisho kinaitwa Kitambulisho cha Mzanzibari Mkaazi. Kwa hivyo, hili neno mkaazi katika nchi hii mkaazi ni nani, kwa sababu atakayekuja pia atakuwa ni mkaazi na Wazanzibari wote ni wakaazi.

Sasa mimi katika hili nilikuwa nataka nimshauri Mhe. Waziri badala ya kuita Kitambulisho cha Mzanzibari Mkaazi akiite Kitambulisho cha Mzanzibari na hili neno mkaazi liondoke, kwa sababu nilimwambia atoe tafsiri ya neno mkaazi hakutoa. *(Makofi)*

Mhe. Waziri wa Nchi, (OR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi: Mhe. Mwenyekiti, nafikiri nilijitahidi sana kuzungumza nani Mzanzibari na nani Mzanzibari Mkaazi, na hata siku nilipotoa maelezo yangu ya kwanza, lakini naomba nisisitize tena nani Mzanzibari Mkaazi. Mzanzibari Mkaazi ni mwenye sifa ya Mzanzibari kama ilivyofafanuliwa katika Sheria Nam. 5 ya mwaka 1985 na pia awe ametimiza sharti ya makaazi ya kudumu Zanzibar. *(Makofi)*

Mhe. Suleiman Hemed Khamis: Mhe. Mwenyekiti, bado sijaridhika na maelezo haya kwamba neno mkaazi kutiwa kwenye Kitambulisho cha Mzanzibari, kwa sababu inakuwa sasa sisi sote ni wakaazi na wale wengine wote watakaokuja, ambapo kwa maelezo wametambulishwa kuwa ni wakaazi wa muda, yaani *temporary resident and permanent resident* na wote ni wakaazi.

Kwa hivyo, hili neno wakaazi kwa hapa kwa nini lisiondolewe hili neno na kuitwa Kitambulisho cha Mzanzibari na huu ukaazi una maana gani. Vile vile kwa tafsiri nyengine hii ni kuonesha kama kutoa mwanya kwa watu wengine ambao watakaokuja kama ni wakaazi wapate uthibitisho wa Uzanzibari ndio maana yake. Mhe. Mwenyekiti, mimi napenda neno mkaazi liondoke kabisa na kiitwe Kitambulisho cha Mzanzibari inatosha.

UTARATIBU

Mhe. Ussi Jecha Simai: Mhe. Mwenyekiti, kuhusu utaratibu kifungu cha kwanza ambacho Mhe. Mjumbe ambacho anakilalamikia tayari tumeshakipitisha, kwa sababu aliponyanyuka yeye ilikuwa tayari kifungu kimeshapita. Kwa hiyo, hakuna haja ya kujadiliwa tena hicho tusubiri mambo mengine huko mbele. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti: Mimi nilichoona yeye aliulizia kifungu cha pili kusomeka, yaani ukisoma kifungu cha pili hiyo mkaazi ipo tena ndipo alipoulizia. Mhe. Waziri wa Nchi, (OR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi. *(Makofi)*

Mhe. Waziri wa Nchi, (OR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi: Mhe. Mwenyekiti, nafikiri kama ulivyosema kwamba kwenye kifungu cha pili ipo maana kwa mujibu wa sheria hii, kidogo tusichanyanye nafikiri kama alivyoelezea Mhe. Suleiman Hemed Khamis *citizen* na *resident* aa! Mimi sitaki kwenda kwenye Kiingereza isipokuwa tuchukue hii ya Kiswahili kwanza.

Kwa hivyo, namuomba Mhe. Mjumbe afungue hapo aliposema kwenye kifungu cha 3(c) kwa kuongeza ufafanuzi wa maneno yafuatayo Mkaazi asiyekuwa Mzanzibari, maana yake ni mtu yeyote mbali ya mkaazi wa muda wa Mzanzibari Mkaazi ambaye ameingia na anayeishi kisheria, tayari tumeshamu-*identify* Mzanzibari Mkaazi ni nani, na Mzanzibari jana nilisema kwamba wako kwa *categories* mbili, yaani wale wa kuzaliwa na wengine na tuliwataja.

Lakini huyu mkaazi lazima awe Mzanzibari, ili ndio tunampa huo Uzanzibari Ukaazi na kama nilivyosema kwamba wametapakaa Wazanzibari kwa kuzaliwa, yaani wako wengi nje huko lakini wale hatuwezi kuwapa fursa za Uzanzibari wakati wako nje, isipokuwa waje nyumbani na wafuate masharti tutawasajili wawe wa kudumu na hiyo ndiyo tofauti yenyewe.

Mhe. Suleiman Hemed Khamis: Mhe. Mwenyekiti, kwa suala hili uraia hatuna kwa sababu ameshasema yeye kwamba raia ni wa Tanzania, lakini mkaazi kwa suala hili itakuwa haliingii hapa, hivyo ni vyema kusema Kitambulisho cha Mzanzibari na raia ni Mtanzania kama alivyosema kwa sababu ni ya Muungano. Lakini hapa akisema mkaazi ni kama tunajigonga kwenye maelezo na wala hakuna sababu za mkaazi hapa, isipokuwa Kitambulisho cha Mzanzibari khalas imemaliza. *(Kicheko/Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti: Waheshimiwa Wajumbe, tunafanya nini. Nadhani jambo la kufanya ehe! Mhe. Waziri wa Nchi, (OR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, kuna maelezo zaidi.

Mhe. Waziri wa Nchi, (OR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi: Mhe. Mwenyekiti, jana Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa jana alisoma *hansard* nzuri sana iliyofafanuliwa kwa urefu kuhusu maana hii, tena ni *hansard* ya nyuma kabisa. Kwa hivyo, namuomba baadaye akaitafute kwa ajili ya kupata maelezo sahihi.

Mhe. Mwenyekiti, naomba kurudia tena kumfahamisha Mhe. Suleiman Hemed Khamis, unajua hapa lazima tuende kwa mujibu wa sheria hii na wala usitafsiri *in general terms* aa! Uende kwa mujibu wa malengo yetu ya sheria yanavyosema. Sasa ukitafsiri kwa ujumla tu hai-*apply* kwenye sheria yetu.

Kwa kweli sheria yetu inavyoelekeza na tumetafsiri na tumesema huyo mkaazi tunamkusudia nani kwa mujibu wa sheria hii, na tukatoa kielelezo chake kwamba awe wa kudumu. Kwa maana hiyo, yule ni Mzanzibari ni sawa kabisa, lakini wa kudumu ndiye tunayem-*qualify* hapa na ndiye iliyemtaka.

Sasa huwezi kusema kwamba wote hawa ni kweli wapo Wazanzibari nje huko, lakini wanavyo vitambulisho hivyo vya Mzanzibari, wengine huko nje hawana sasa tuwape vipi na tuwaambie Vitambulisho vya Mzanzibari na tumtafute wa Denmark, Muscat, Oman pamoja na nchi nyengine. Kwa hivyo, kazi hiyo ndio nikasema pale hilo zoezi ni gumu mno na wala halitekelezeki.

Kwa hiyo, nasema Mhe. Suleiman Hemed Khamis atafautishe *the real terms* tafsiri ya neno mkaazi na yule tuliyemkusudia au tuliyem-*define* hapa kwenye sheria.

Mhe. Mwanasheria Mkuu: Mhe. Mwenyekiti, inawezekana Mhe. Suleiman Hemed Khamis anayo hoja ya msingi, lakini mambo yetu hapa ndio maana Mhe. Mwenyekiti umeteremka kutoka juu kama Spika, na hivi sasa uko hapo kama Mwenyekiti ni kwa sababu ya utaratibu.

Sasa tunachojadili katika mswada huu ni marekebisho ambayo yameletwa na marekebisho haya ambayo yameletwa hakuna suala la kubadilisha kifungu cha pili cha sheria mama, ambacho kinatafsiri mkaazi, maana yake hiyo tafsiri ya mkaazi ipo kwenye sheria mama katika kifungu cha pili na humu hakuna marekebisho hayo na wala haipendekezwi kuliondoa na kubadilishwa.
Lakini Kanuni zetu zinamruhusu Mjumbe kupendekeza marekebisho, kwa sababu marekebisho ambayo yeye anapendekeza yatabadilisha kwa kiasi kikubwa sio tu huu mswada, lakini hata na sheria yenyewe Kanuni yetu ya 84 inaelekeza utaratibu wa kufanya hivyo, kwamba ilikuwa alete kwa maandishi na ayakabidhi kwa Katibu.

Mhe. Mwenyekiti, kwa kuwa Mhe. Suleiman Hemed Khamis kwa kuwa hakufanya hivyo, mimi nasema inawezekana anayo hoja ya msingi sana, lakini kwa sababu huu utaratibu haukufuatwa, basi mimi naomba Mhe. Mwenyekiti tuendelee kwenye hili. *(Makofi)*

Mhe. Suleiman Hemed Khamis: Mhe. Mwenyekiti, ikiwa ni suala la Mzanzibari Mkaazi na katika suala hili na kwenye sheria haijasema cheti cha kuzaliwa, ni mtu ambaye inasema uthibitisho au utambulisho ni kitu chochote inaweza kuwa kadi ya skuli au gamba la hospitali au kadi ya uraia ya zamani ama *passport* na vyote ni vitambulisho. Sasa haijasema kwamba lazima kiwe cheti cha kuzaliwa na hamna kwenye sheria, naomba jibu katika swali hilo.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Mjumbe, sasa ni hoja nyengine ya cheti cha kuzaliwa au vipi. Nafikiri tuendelee.

Mhe. Suleiman Hemed Khamis: Mhe. Mwenyekiti, mimi nimeshamaliza.

Mhe. Mwenyekiti: Waheshimiwa Wajumbe, nadhani tuendelee, kwa sababu sheria yenyewe inahusu Mzanzibari Mkaazi na maelezo yake awe wa kudumu, tena Mhe. Waziri ametoa wito hapa kama kuna wengine huko wakija katika kipindi cha mwezi mmoja basi anaweza kujisajili kuwa ni Mzanzibari Mkaazi, kama atakuwa na makaazi ya kudumu. Tunaendelea. *(Makofi)*

Kifungu 2 – Kusomeka

Sehemu ya Pili

Marekebisho

Kifungu 3 – Marekebisho ya kifungu cha 2
Kifungu 4

Mhe. Asaa Othman Hamad: Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru wakati nilipokuwa nikichangia eneo hili nililalamika kwa jinsi gani Sheha wa Shehia ya Utaani ndani ya Jimbo langu la Wete anavyowanyima za kuwapa barua kupata vitambulisho vijana wa shehia yake. Hili Mhe. Waziri katika kufafanua hakulitaja. Neno la pili nashukuru amelitaja na ametoa majibu ambayo sikuridhika hata kidogo ya hawa 'Ubaya Ubaya'

Mhe. Mwenyekiti, vijana wanaonyimwa barua na Sheha huyu Massoud *Roho Mbaya* wa Wete ni vijana wakati yeye anafanya kazi ya polisi ni nyumba ya tatu kutoka nyumba yake wanasoma Utaani, wanahitimu pale Utaani. Leo jibu ni rahisi kwake anasema sina fomu, hasemi siwatambui. Sina fomu inatosha kwake kuwa hawa hawana pengine pa kwenda. Lakini hatuamini kwamba ni sababu ya msingi kweli kwamba hana fomu.

Mhe. Waziri asikinge kifua kwa watu wengine, akinge kifua kuitetea sheria, sheria haina tatizo, watu wake ndio wenye tatizo. Sasa kama anakinga kifua kwa watu kama hetu ataje utaratibu ambao utathibitisha haya ninayoyasema, mimi niko tayari kumchukua yeye na watu wake wa vitambulisho mpaka Wete. Endapo haya ninayoyasema yatathibitika si sahihi Mhe. Spika, nitachukua hatua mimi mwenyewe kwa kulidanganya Baraza hili. Hilo la kwanza.

La pili kundi la 'Ubaya Ubaya' Mhe. Mwenyekiti, sikuridhika na kauli ya Mhe. Waziri kwamba wanakwenda kujipanga wakati watu wanaathirika na watajipanga hadi lini? Vyote nilivyovitaja jana JKU, KMKM, KV, Polisi, kundi lile lishindikane mpaka serikali iende kujipanga. Mhe. Mwenyekiti watu wanafunga maduka hawafanyi shughuli zao za kupata rizki. Mtu anashushwa vespa, anamrudisha mama hospitali saa 4:00 ya usiku anaambiwa tupe vespa au tupe mama huyo. Anaiwacha vespa anaondoka na mke wake hali hii imeshafika hivyo, juzi barabarani, mapanga yanachezeshwa pale watu wanakimbia, maduka wanayawacha hivi hivi. Serikali inakwenda kujipanga, serikali haijatupa jibu ni hatua gani sahihi za dharura katika hali hii ili Wazanzibari wapate imani na matumaini na serikali yao kwamba ipo na inawajali na inawathamini.

Mhe. Mwenyekiti, hao polisi duka linavunjwa, kijana kapatikana ni huyu, kumbe baba ake OCD asubuhi anatembea barabarani. Kama kuna ukweli serikali inataka kuchukua hatua inifuate twende nikawapeleke leo hii. Lakini anasimamishwa mwenye gari, kiyoo cha gari kimevunjwa kwa kuwa hakukubali kuwapa pesa hawa vijana. Karudi polisi, polisi wamemfuata wamechukua gari ya raia, wamekwenda polisi kupiga risasi wengine wamekimbia mmoja kakamatwa, asubuhi anatroti na wenzake pale pale. Wananchi wajenge imani wapi sasa au itangaze serikali wananchi wachukue hatua mikononi mwao maana serikali imeshindwa. Atamke Mhe. Waziri hilo.

Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi: Mhe. Mwenyekiti, nafikiri nilieleza kwenye majumuisho yangu kwamba mapungufu ya kiutendaji yapo hatuyakatai. Sasa nilisema kama walivyoniomba twende mimi nimekubali tutakwenda. Hili Mhe. Assaa alipolitaja *specific case* hasa hii mimi namuahidi kwamba tutakwenda pamoja ukiyumkini bora tulifanye haraka sana, twende tukazungumze. Na huyo Sheha aliyemtaja na yeye katika Semina alikuwepo kwa hiyo dozi ya nini serikali inataka ifanye naamini keshaipata.

Sasa likatoka azimio kabisa kwamba masheha wote wanapaswa wafate taratibu ziliopo kutoa vitambulisho wasizuie haki za watu. Kwanza nataka kusema dozi ya agizo la serikali ni imani yangu kwamba Sheha huyu keshaipata. Mimi namuomba sana Mhe. Assaa mimi nakubali mapungufu haya lakini tutayafatilia pamoja mimi na yeye twende tukaweke sawa haki za vijana ziwepo.

Kuhusu suala la 'Ubaya Ubaya" Mhe. Asaa jana alitwambia na sisi kama alivyosema tumeipata. Lakini tunavyosema tujipange ni lazima tujipange, kujipanga kwa serikali si lazima wimbi mbili, tatu, hapana. Siku moja tu, jana ile tulivyotoka hapa sisi tukaanza kujipanga jana. Hatua za *operational* ni lazima ujipange huwezi kwenda kibububu, wale wana mapanga, hawana Msalie Mtume, usipojipanga ukenda hivi hivi tu, utapigwa mapanga wala hujui panga linatokea wapi. Mimi nimetumia neno la kwenye mabano tujipange na sisi tuwakabili vipi, tukende na bunduki tutawauwa wote wale halafu itakuja kuwa kesi nyengine hapa. Lazima tujipange tujue tunawaingia vipi, wao wamejidhatiti wale, hawajali wanakwenda panga kiunoni.

Mhe. Asaa sasa tusipojipanga wanaweza wakakupiga panga, maana wale ubaya wao wanafanya mchana mchana ni kweli kabisa. Sisi kama serikali nasema tumelisikia Mheshimiwa na tutalifanyia kazi haraka iwezekanavyo tena nasisitiza haraka iwezekanavyo. Sote tunaumwa, hapa jana wakati tunafanya majumuisho nimepigiwa simu mfanyakazi wako mmoja wakati anarudi kazini karushiwa panga, kaambiwa asimame hakusimama, wakamrushia mpanga limevunja kiyoo.

Hatukatai *concern* ya Mhe. Asaa kama serikali nasema siwezi leo hii kusema vikosi fanyeni hivi, kwanza mamlaka hayo sina tuwaachie wenyewe Makamanda tuone wanafanyaje tujue, upesi upesi haraka iwezekanavyo. Na hii kwenda kwenye *specific case* nakubali tutakwenda kuishughulikia pamoja na hili tutalifanyia kazi haraka iwezekanavyo. Nakubali malalamiko aliyoyapata kwa wananchi. Ahsante.

Mhe. Mwenyekiti: Nilikuwa naogopa sana kwamba Waziri atoe kauli kwamba wananchi wachukue sheria mikononi mwao. Hii ni hatari, kauli kama hiyo kwamba itoke kwenye chombo cha kutunga sheria chombo ambacho tuko viongozi, hapana hiyo nilikuwa namsubiri tu nimwambie hapana hiyo usije ukatoa na kwa kweli haiwezi kutoka kauli kama hiyo. Huo tena utakuwa sio uwongozi ni vurugu.

Mhe. Hijja Hassan Hijja: Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru na kwa niaba ya wananchi wa jimbo la Kiwani kwanza nisikitike sana…

Mhe. Mwenyekiti: Hebu Mhe. Hijja Hassan samahani kidogo. Mhe. Asaa sikukurudia kwa sababu hichi kifungu kama ulivyoelezea kwamba sheria haina matatizo isipokuwa ulichokuwa unataka kujua Waziri atachukua hatua gani kwa mambo mbali mbali. Kwa hiyo ameshaeleza hayo na ndio maana sikukurudia kwamba unaonaje. Lakini maelezo ameshatoa mtakwenda huko na ndio maana nikachukua hoja ya pili ya Mhe. Hija.

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Mwenyekiti, mimi nikushukuru lakini kwa masikitiko makubwa kwa niaba ya wananchi wa jimbo la Kiwani kwamba leo serikali yetu inaogopa mapanga wakati wana vikosi na mizinga na mabunduki kwa kweli ni jambo la aibu sana. Sasa imekuwa wenye mapanga wanatisha kuliko wenye bunduki.

Lakini niseme hoja yangu ya msingi baada ya masikitiko hayo ambayo mimi nashangaa sana ni kwamba kifungu cha 4 tumeongeza kifungu cha 6(a) cha sheria hii mpya tumerekebisha kuongeza kifungu cha 6(a). Inaelekea kifungu hiki kinataka kukidhi matakwa ya wale wageni ambao wamekuja hapa ama kwa taasisi za umma, biashara ama kazi za kujipatia kipato.

Mhe. Waziri alipokuwa akitoa takwimu ambazo za kuchekesha ametwambia kwamba ameandikisha watu laki tano hamsini na saba elfu, mia tisa na hamsini na nne (557,954). Sasa naomba atuwekee wazi basi wale wageni waliokuja hadi leo kwa takwimu hii ambao wapo hapa kwa taasisi za umma kwa maana ya misikiti, makanisa na mambo mengine, wapo hapa kwa ajili ya kazi na biashara labda zile za nyungo na dawa za mbu, atwambie ni wangapi kati hii laki tano ili takwimu ikae sawa.

Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi: Mhe. Mwenyekiti, kwa kweli takwimu hiyo anayoitaka Mhe. Hija Hassan Hija, uchambuzi huo hatukuufanya. Mimi nafikiri baada ya marekebisho haya, tukianza zoezi la kuwasajili wageni na wengineo tuliowasema basi nafikiri takwimu zitaweza kupambanuka. Lakini mimi nimekupa figa za usajili wote tulioufanya na wale wengine ambao nimesema tumewasajili lakini vitambulivyo navyo nao vipo.

Tumeuwona ule ugumu na ndio maana tukaja na marekebisho haya. Nafikiri marekebisho haya tukiyafanya tutaweza kuwabaini. Lakini kwa figa alizoshauri Mheshimiwa kwa kweli hizo sina.

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Mwenyekiti, kama utakumbuka Mhe. Waziri ametwambia hapa kwamba kuna kesi 19 za watu ambao wamekamatwa. Mimi ninazoripoti hapa mbali mbali kwamba miaka yote hiyo ya sheria hii ilipoanza ya vitambulisho hadi hii leo Wizara yake imekamata watu 19 tu, hapo kitu hicho kimenishangaza. Wakati ukweli ulivyo takwimu za wageni walioingia hapa na jana nilisema hapa kwamba wengi wamevamia soko la ajira ya Mahoteli na wanajulikana kwa majina na tumewapa dhamana kubwa kwenye mahoteli hayo.

Mhe. Mwenyekiti, kuna ugumu gani kwa serikali kwenda kuwatoa. Kwa sababu kwanza wameingia kinyume na sheria, wameghushi vyeti vya kuzaliwa, wameghushi Zanzibar ID na wanajulikana. Kuna ugumugani wa SMZ

kwenda kuwatoa ili wananchi wetu wa Zanzibari kujenga imani kwamba serikali yao kweli inawajali wazalendo kuliko wageni. Leo anatwambia watu 19 ndio waliokamatwa tena wanachunguzwa. Maana yake miaka saba ya sheria watu 19 wanachunguzwa.

Ninachoona mimi kwa upande wangu kwamba hii sheria kifungu hiki kinataka kuwahalalisha wale wote ambao wameingia ambao kwa mtazamo wangu ni zaidi ya elfu mbili. Sasa hebu Mhe. Waziri atwambie kuna ugumu gani kuwatoa wale watu ambao wanajulikana kwamba huyu ni PO hoteli fulani, Mrwanda, Mkenya, ameingia hapa kwa kughushi cheti au atwambie wameridhiwa kwa misingi gani.

Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi: Mhe. Mwenyekiti hakuna ugumu wowote ni suala la taratibu tu. Unajua haya mambo ni lazima twende hatua kwa hatua. Mimi namshukuru kwamba anao watu ambao anahisi yeye wameingia nje ya kitaratibu na wanaishi. Ningemuomba baadaye atusaidie hizo. Namuhakikishia kwamba hilo tutalifanyia kazi.

Sote tunatakiwa tuwe raia wema wa kuilinda nchi yetu na hasa kwa wale wanaokhalif sheria. Jambo hili unapata mwengine kwenye *source* hii mwengine *source* hii lakini sote ni walinzi wa nchi yetu. Kwa hiyo, mimi nakubali kabisa anavyoelekeza Mhe. Hija na hakuna ugumu wowote. Tutamfata yeye atupe hivyo vielelezo, na waheshimiwa wengine wowote nawaomba kama wapo watu wanaowafahamu basi watusaidie majina, ili tuwafatilia.

Nasisitiza tena hili zoezi tukilianza nafikiri litatusaidia na hao wengine ambao tunasema wanafanya kazi mahoteli na mambo mengi, wengine wana vyeti vya Uzanzibar hilo ndio itatusaidia sana kuwabaini. Nafikiri marekebisho haya tukishaidhinisha yatatusaidia sana, huo ndio mtazamo wangu Mheshimiwa. Namuomba sana Mheshimiwa yeye na wengine atuletee tutayafanyia kazi hakuna ugumu.

Mhe. Mwenyekiti: Nafikiri tuendelee. Na kama nilivyosema kama kuna mjumbe yeyote au hara raia mwengine anahisi kwamba kuna watu wameingia ndani ya nchi kinyume na utaratibu na wanakaa kinyume na utaratibu ni kuripoti kunakohusika. Huo kwa kweli ni wajibu wa kila Mzanzibari. Mimi natoa mfano mmoja.

Kuna siku moja nilikwenda Benki kutafuta fedha nikakutana na watu ambao ni wageni, masuala yao waliyoniuliza mimi nikapata wasi wasi. Nikafanya rai nikaingia nao ndani ya gari moja kwa moja mpaka *Immigration* nikawambia hapa ulizeni maswali na hawakurudi. Kumbe walikuwa wameingia isivyohalali. Kwa huo ni wajibu wa kila Mzanzibari kulinda nchi yake. Nadhani tuendelee.

Mhe. Salim Abdalla Hamad: Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Waziri aliponijibu swali langu alitumia kifungu cha 16 cha sheria mama ambacho kwa ruhusa yako naomba nikisome kama ifuatavyo,

> Kifungu Nam 16. *"Power to make regulations*
> *The Minister may make rules, orders or regulations not inconcistant with the provision of this Act for the batter carrying out the provisions of this act."*

Lakini mimi sicho kifungu nilichozungumza katika hoja yangu.

Mhe. Mwenyekiti, kifungu Nam. 4 cha Mswada huu tunaoufanyia marekebisho kinaeleza kuwa kifungu cha 6 cha sheria mama kimefanyiwa marekebisho kwa kuongeza kifungu kipya cha 6(a) mara baada ya kifungu cha 6 kama ifuatavyo:-

Sasa kabla sijasema kama ifuatavyo nilikiangalia hicho kifungu cha 6 na kifungu cha 6 Mheshimiwa kwa ruhusa yako naomba nikisome kifahamike halafu nilete hoja yangu. Hichi kifungu cha 6 maneno ya pembeni kimeandika hivi *"Duties of the director of registration"* na kifungu chenyewe kinasema hivi:

> *"Subject to the provision of this act and directives of the minster the director shall no (1) register every Zanzibari resident in Zanzibar who has attained the age of 18 years and above ……?"*

Kwa sababu ya maana ya kifungu hichi nilivyofahamu mimi nikuwa pamoja na sheria iliyokuwepo lakini *and directive of the minister* inaandikwa hivyo na maelekezo ya Waziri, tena *director* ndio wanaofanya haya mambo. Kwa hivyo hawezi akafanya kwa kufuata sheria tu, lakini pia anafuata maelezo ya Waziri. Kwa maana hiyo mimi

nimeangalia sana namna tunavyopata dhiki ya watu kupewa hizi haki zao. Hakuna watu waliokuwa wanatuharibia kama Masheha, huyu waziri mwenyewe ndiye mwenye Wakuu wa Mikoa yeye ndiye anayechagua masheha. Lakini hatujasikia hata mmoja kuwa masheha kwa kukiuka sheria kuchukuliwa hatua na wakati anawakosesha watu haki zao. Ndio nikasema hizi *directive* ndizo zinazosababisha sheha aweze kutuharibia mambo yetu mpaka ikaonekana kuwa haki haitendeki. Naomba jibu.

Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi: Ni kweli Mhe. Mwenyekiti, aliuliza hiyo hoja na nilimjibu kwamba hapa *directives* iliokusudiwa sio kwamba Waziri atoe kinyume na maelekezo. Hapa kama nampa *authorization* inampa mamlaka Mkurugenzi, sio kama mimi nitatoa maagizo mengine ya nje. Inajua lugha ya kisheria, mimi sio mwana sheria, lakini ninachokusudia hapa *directives* zenyewe ndio hizo moja mbili tatu. Sitoi nje ya hizi tatu, wala sitotoa kinyume na maelekezo haya. Masheha ni kweli wapo kwenye Wizara yetu lakini na sisi hatutowaachia Shesha wafanye mambo nje ya utaratibu, si kweli.

Binaadamu katika utekelezaji tupo tofauti lakini hilo tumeshalisimamia. Nasisitiza tena semina tuliyoifanya juzi Mhe. Mwenyekiti Pemba ilikuwa nzuri sana, tume *interrupt* vizuri sana, Masheha wote na madiwani wote wa Pemba kila shehia na tumewaelekeza nini wajibu wao. Ikiwa bado kuna sheha atakwenda kinyume na taratibu za nchi mimi namuomba Mhe. Salim Aballa atwambie tuona hatua za kumchukulia kama yupo kweli ambaye anafanya hayo. Ahsante.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Salim Abadalla maelekezo ya Mhe. Waziri kuna Masheha wanaokwenda kinyume na taratibu za sheria hii basi umpelekee ili ionekane makoseo yao yako wapi.

Mhe. Salim Abdalla Hamad: Mhe. Mwenyekiti, lakini kwa bahati mbaya mimi si mwana sheria, haikunionesha katika sheria kuwa lazima *direct* atakazotoa Mhe. Waziri ziendane na mkataba huo, hivyo haikueleza, ile ni shauri yake mwenyewe. Ninachosema kwanini itokezee matatizo kwa masheha tu, wakati hawa watu wapo kwenye mamlaka yake na hatujaanza leo siku zote tunapiga kelele.

Mimi ushauri wangu kwa kuondoa matatizo na Mhe. Waziri kujiweka safi ni kutafuta utaratibu ambao sheha asihusike hasa katika haki za wananchi kama hizi ambazo kwa makusudi anatuharibia. Juzi kulikuwa na usajili wa Sensa lakini masheha walifanya kazi nzuri sana. Ina maana wanatufanyia makusudi wala hakuna aliyechukuliwa hatua, si Mhe. Waziri wala si Mkuu wa Wilaya wala wa Mkoa. Lakini kwa upande mwengine utamuona sheha yule yule anaendelea na watu mpaka leo wamekosa haki zao. Kunambia miye nikawatafute niwaletee, si sheria wala haielekei, mimi kazi yangu si kutafuta watu waliokoseshwa haki nikawaleta hapa. Waziri aone kuwa haki inatendeka ndilo alilowekewa hapo.

Mimi ushauri wangu Mhe. Spika, kwa vile ni tatizo akitaka ushahidi nitamletea. Mimi naomba tusiitie serikali yetu katika matatizo kwa jambo ambalo sio la lazima. Huu Mswada hauna tatizo lolote lakini utekelezaji wake haufanywi inavyotakiwa. Kwa maana hii basi Mheshimiwa angalitupa ushauri mwengine japo sisi na madiwani tukashirikishwa katika kuwatetea wananchi na ataona mambo yatakavyokwenda. Kuliko kumuamini sheha ambao wanatuharibia kwa makusudi wala hakuna hatua zinazochukuliwa.

Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi: Mhe. Mwenyekiti, mimi ningemuomba Mhe. Salim kama nilivyotoa ahadi kwengine, inaelekea ana *specific* masheha. Mimi ningemuomba tukitoka hapa tupange mimi nakubali kabisa tutajitahidi na watendaji wangu wananisikia wa Kitengo cha Usajili, twende tufatilie tuone matatizo yako wapi ili tuwaweke sawa, hakuna matatizo. Hilo tutajitahidi Mheshimiwa na namuahidi mbele ya Baraza lako tukufu hilo tutalitekeleza.

Kifungu cha 4 Kuongeza kifungu kipya cha 6(a) pamoja na marekebisho yake.

Mhe. Mwenyekiti: Hii tena Mheshimiwa ukae. Maelezo keshatoa kama kuna masheha *specific* wanao matatizo, panga nae umpelekee matatizo yajulikane ili aweze kuchukua hatua na aweze kutoa maelekezo. Mimi nadhani tuendelee Mheshimiwa. Ombi.

Mhe. Salim Abdalla Hamad: Ombi langu hili ni la Wazanzibari wote na sio kwa jimbo la Mtambwe tu. Kwa hivyo afanye kazi kwa Zanzibar yote. Hilo tu ndio ombi langu na asionane na miye tu tupange kwa sote kwa ratiba maalum ili hili suala lifatiliwe.

Mhe. Mwenyekiti: Wajumbe ambao wana matatizo katika majimbo yao watamwambia Mhe. Waziri tusiseme kwamba wooooote, hapana hiyo itakuwa sio sawa, wengine hawajalalamika.

Kifungu 5 Marekebisho ya Kifungu cha 7 pamoja na marekebisho yake.

Kifungu 6 Marekebisho ya Kifungu cha 10.
Kifungu 7 Marekebisho ya kifungu cha 12
Kifungu 8 Marekebisho ya kifungu cha 14

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vimepitishwa na Kamati ya Kutunga Sheria pamoja na marekebisho yake)

(Baraza linarudia)

Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi: Mhe. Spika, ilivyokuwa Kamati ya Kutunga sheria imeupitia Mswada wangu kifungu kwa kifungu pamoja na marekebisho yake na kuukubali pamoja na marekebisho yake. Sasa naliomba Baraza lako tukufu liukubali naomba kutoa hoja.

(Hoja imetolwa iamuliwe)

(Hoja imeamuliwa na kuafikiwa)

Mswada wa Sheria wa Usajili wa Mzanzibari Mkaazi (Marekebisho) ya Mwaka 2012

(Kusomwa kwa mara ya tatu)

Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi: Mhe. Spika, naomba kutoa hoja kuwa Mswada wa Sheria wa Usajili wa Mzanzibari Mkaazi ya marekebisho ya mwaka 2012, usomwe kwa mara ya tatu.

(Hoja imetolewa iamuliwe)
(Hoja imeamuliwa na kuafikiwa)

(Mswada wa Serikali umesomwa mara ya tatu na kupitishwa)

Katibu: Mhe. Spika, naomba kutoa taarifa kwamba Mswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria ya Usajili wa Mzanzibari Mkaazi Nam. 7 ya mwaka 2005 na mambo mengine yanayohusiana na hayo, sasa umepitishwa rasmi na Baraza lako la Wawakilishi uwe ni sheria. *(Makofi)*

Mhe. Spika, naomba kutoa taarifa kuwa kwa mujibu wa orodha ya shughuli za leo hapa ndio mwisho wa shughuli zetu.

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe kwanza naomba nichukue nafasi hii kuwashukuru sana kwa kazi kubwa ambayo tumeshirikiana kuifanya mpaka hapa tumeimaliza. Leo kimsingi ilikuwa baada ya shughuli hii tuendelee na Wizara ya Afya lakini Waziri yuko safirini na kesho ndio rasmi tunategemea atakuwa yupo tayari. Ndio maana kwa leo ikawa baada ya hapa hakuna shughuli nyengine. Naomba kabla ya kusitisha shughuli zetu nitoe taarifa fupi sana.

Waheshimiwa Wajumbe naomba kutoa taarifa kwa waheshimiwa wawakilishi wanawake kwamba yale mafungu ya Wawakilishi wanawake yatakuwa yanaendelea leo hii mara baada ya kuakhirisha shughuli zetu. Waheshimiwa Wawakilishi wanawake wanajua mafunzo hayo wanayafanyia wapi baada ya shughuli hizi mkaendelee na kazi hiyo.

Baada ya hayo Waheshimiwa Wajumbe naakhirisha kikao hichi hadi kesho tarehe 18, Oktoba 2012, saa 3:00 za asubuhi.

(Saa 5:30 asubuhi Baraza liliakhirishwa hadi tarehe 18/10/2012 saa 3:00 asubuhi)